**KENYA INSTITUTE OF CURRICULUM DEVELOPMENT**

A Skilled and Ethical Society

# STASHAHADA YA UALIMU WA SHULE YA CHEKECHEA NA MSINGI.

# MTAALA WA KISWAHILI

# 2024

Toleo la Kwanza 2021

Toleo la Pili 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

**ISBN:** 978-9914-724-68-4

Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

**TABLE OF CONTENT**

UTANGULIZI………………………………………………………………………………………………………………… v

KANUNI NA MAHITAJI YA KUJIUNGA NA STASHAHADA YA UALIMU WA SHULE YA MSINGI NA CHEKECHEA (DTE- PP&P)………………………………………………………………………………………………………………... vii

MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA………………………………………………………………........ xiv

MTAALA WA STASHAHADA YA UALIMU WA SHULE YA MSINGI NA CHEKECHEA…………………………………. xvii

KAULI KIINI…………………………………………………………………………………………………………………. xvii

MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA MAFUNZO YA KISWAHILI YA STASHAHADA YA UALIMU WA SHULE YA MSINGI NA CHEKECHEA………………………………………………………………………………... xvii

DRAFT

**UTANGULIZI**

Ukuzaji wa mtaala wa Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi na Chekechea (DTE-PP&P) ni hatua muhimu katika utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi (CBC) nchini Kenya. Mtaala huu umekuzwa ili kumwandaa mkurufunzi kuweza kumwelekeza kikamilifu mwanafunzi wa kiwango cha shule ya msingi na Chekechea katika Elimu ya Msingi.

Inakusudiwa kuwa mkufunzi atamwelekeza ifaavyo mkurufunzi aweze kukumbatia uhamaji kutoka kwa Mtaala ya unaoegemea maarifa hadi Mtaala wa Kiumilisi ambao nguzo yake ni mbinu zinamzolenga mwanafunzi kwa utimizaji wa matokeo yanayotarajiwa. Zaidi, unasisitiza tathmini endelevu kufanikisha ujifunzaji na kama msingi wa kutathminia mwelekeo na uwezo wa mwanafunzi. Sifa nyingine muhimu ambazo zimeingiwa ni vijizoezi vya kufundishia vya mara kwa mara na muda mrefu wa mazoezi ya shuleni pamoja na kuanzishwa kwa kozi halisi za kitaaluma zinazoambatana na ruwaza, wito, mihimili na kanuni za CBC zilizo katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (KICD, 2017).

DPTE inalenga kumkuza mwalimu kuwa kama mwezeshaji katika mchakato wa ujifunzaji akitilia maanani uwezo tofautitofauti na mitindo ya ujifunzaji ya wanafunzi binafsi wanaolengwa. Mtaala huu umebuniwa ukiwa na msisitizo katika ujifunzaji wa kitajriba na tafakuri ili kukuza mbinu mwafaka za kufundishia maarifa mbalimbali; hii ndiyo maana ya kuwepo kwa msisitizo wa kuambatanisha maarifa na mbinu za kuyafundishia. Lengo ni kuhakikisha kuwa mkurufunzi amepewa muda wa kutosha kujizoeza jinsi ya kuwezesha ujifunzaji wa mada tofautotofauti zilizotolewa katika mtaala.

Mtaala wa Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi na Chekechea (DTE-PP&P) una kozi zifuatazo:

**Kozi za Kitaaluma**

1. Child Development and Psychology
2. Curriculum Studies
3. Educational Resources
4. ICT Integration in Education
5. Educational Assessment
6. Communication and Research Skills
7. Inclusive Education

**Masomo na Ufundishaji**

1. English
2. Kiswahili/KSL
3. Mathematics
4. Science and Technology
5. Agriculture
6. Home Science
7. Religious Education: CRE/IRE/HRE

8. Educational Leadership and Management
9. Sociological and Philosophical Foundations of Education
10. Historical and Comparative Foundations of Education
11. Micro Teaching
12. Practicum

8. Social Studies
9. Physical and Health Education
10. Art and Craft
11. Music
12. Indigenous Language
13. Foreign Languages: French/ Arabic/ German/ Mandarin (Chinese)/ KSL

DRAFT

**KANUNI NA MAHITAJI YA KUJIUNGA NA STASHAHADA YA UALIMU WA SHULE YA MSINGI NA CHEKECHEA (DTE – PP&P)**

Mahitaji ya kujiunga na Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi yatakuwa Gredi C katika Cheti cha Mtihani wa Elimu ya Shule ya Upili Kenya (KCSE) au kiwango sawa na hicho (kama ilivyokadiriwa na KNEC). Waombaji nafasi wenye mahitaji maalumu (SNE) wanaweza kuchukuliwa kwa Gredi ya C- katika KCSE.

**MUDA WA MAFUNZO**

Muda wa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi na Chekechea utakuwa miaka mitatu na chekechea.

**MASOMO YANAYOTOLEWA**

Wanafunzi wa Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi na Chekechea (DPTE) watasoma kozi zote zilizo katika mtaala wa DPTE; ambazo zinajumuisha Kozi za Kitaaluma na masomo yaliyo katika mtaala wa shule za msingi.

**UFUNDISHAJI KATITI NA MAZOEZI YA KUFUNDISHIA**

Ufundishaji katiti utafanyika kama kozi ya lazima kabla ya mazoezi ya shuleni; hivyo, kozi hiyo imebuniwa. Kutakuwa na mihula miwili (2) ya mazoezi ya kufundishia shuleni na ambayo mwongozo wake utatolewa.

**UTUZAJI WA STASHAHADA**

Ili kutuzwa Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi, mtahiniwa lazima atimize yafuatayo:

i) Akamilishe muda uliotolewa wa kozi na afaulu tathmini itakayotolewa kama ilivyoelezewa na Baraza la Kitaifa la Mitihani Kenya (KNEC).

ii) Akamilishe muda unaohitajika wa mazoezi ya shuleni na afaulu tathmini itakayotolewa kama ilivyoelezewa na Baraza la Kitaifa la Mitihani Kenya (KNEC).

DRAFT

Tanbihi: Ikiwa mwanafunzi hakuweza kutimiza mahitaji ya kutolewa kwa Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi, ataruhusiwa kurudia kipengele halisi au somo ambalo hakufaulu.

**GREDI**

Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi itakuwa na gredi zitakazotolewa na Baraza la Kitaifa la Mitihani Kenya (KNEC).

DRAFT

## JEDWALI 1: MGAO WA KOZI ZA KITAALUMA

| | Masomo | Muhula 1 | Muhula 2 | Muhula 3 | Muhula 4 | Muhula 5 | Muhula 6 | JUMLA | Muhua 7 Ufundishaji Katiti | Muhula 8 | Muhula 9 | Jumla Kwa Kozi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **KOZI ZA KITAALUMA** | | | | | | | | | | | | **KOZI ZA KITAALUMA (SAA 420 )** |
| 1. | Child Development and Psychology | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 60 | | | | |
| 2. | Curriculum Studies | 30 | 20 | 20 | 20 | | | 90 | | | | |
| 3. | Educational Resources | 10 | 10 | 10 | | | | 30 | | | | |
| 4. | ICT Integration in Education | 10 | 10 | 10 | | | | 30 | | | | |
| 5. | Educational Assessment | 10 | 10 | 10 | | | | 30 | | | | |
| 6. | Research Skills | 10 | 10 | 4 | | | | 24 | | | | |
| 7. | Inclusive Education | 10 | 10 | 10 | | | | 30 | | | | |
| 8. | Educational Leadership and Management | | | | 10 | 10 | 10 | 30 | | | | |
| 9. | Sociological and Philosophical Foundations | | | | 10 | 10 | 10 | 30 | | | | |

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | of Education | | | | | | | | | | | |
| 10. | Historical and Comparative Foundations of Education | | | | 10 | 10 | 10 | 30 | | | | |
| 11. | Micro Teaching | 30 | | | | | | 30 | | | | |
| **JUMLA** | | **SAA 120** | **SAA 80** | **SAA 80** | **SAA 60** | **SAA 40** | **SAA 40** | **SAA 414** | | | | |

DRAFT

## JEDWALI 2: MGAO WA MASOMO NA UFUNDISHAJI

| **MASOMO + UFUNDISHAJI** | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **MASOMO** | **Muhula 1** | **Muhula 2** | **Muhula 3** | **Muhula 4** | **Muhula 5** | **Muhula 6** | **Jumla** | **Muhula 7 Ufundishaji Katiti** | **Muhula 8** | **Muhula 9** | **Jumla Kwa Kozi** |
| 1 | English | 30 | 30 | 36 | 30 | 30 | 30 | 186 | 30 | **Mazoezi ya ufundishaji<br><br>Saa 300** | **Mazoezi ya ufundishaji<br><br>Saa 300** | **Masomo na ufundishaji (Saa 1680)<br><br>+<br>MAZOEZI YA UFUNDISHAJI (Saa 600)** |
| 2 | Kiswahili /KSL | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 120 | 20 | | | |
| 3 | Mathematics | 30 | 30 | 30 | 30 | 30 | 30 | 180 | 30 | | | |
| 4 | Science and Technology | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 120 | 30 | | | |
| 5 | Agriculture | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 120 | 20 | | | |
| 6 | Home science | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 120 | 20 | | | |
| 7 | Religious Education:- | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 120 | 20 | | | |

DRAFT

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | (CRE, IRE, HRE) | | | | | | | | | | | |
| 8 | Social Studies | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 20 | 120 | 20 | | | |
| 9. | Physical and Health Education | 10 | 10 | 10 | 30 | 30 | 30 | 120 | 30 | | | |
| 10. | Art and craft | 10 | 30 | 30 | 10 | 20 | 20 | 120 | 20 | | | |
| 11. | Music | 10 | 20 | 20 | 20 | 20 | 30 | 120 | 20 | | | |
| 12. | Indigenous Languages | 10 | 20 | 20 | 20 | 30 | 20 | 120 | 20 | | | |
| 13 | Foreign Languages: French/ Arabic/ German/ Mandarin | 10 | 10 | 10 | 30 | 30 | 30 | 120 | 20 | | | |

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | (Chinese)/ KSL | | | | | | | | | | | |
| **IDADI** | | **Saa 230** | **Saa 270** | **Saa 270** | **Saa 290** | **Saa 310** | **Saa 310** | **Saa 1686** | | | | |
| **JUMLA** | | **350** | **350** | **350** | **350** | **350** | **350** | **2100** | **300** | **300** | **300** | **3000** |

DRAFT

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

**Elimu nchini Kenya inatakiwa:**

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa.**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana itakayowezesha jamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia uhai wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**.
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa nchi kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.

   a) **Mahitaji ya kijamii**
   Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mapinduzi kimyakimya ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   b) **Mahitaji ya kiuchumi**
   Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika na wa humu nchini.

   c) **Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
   Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda.

Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**.
   Elimu inapaswa kumwezesha mtu kutambua, kupalilia, kukuza na kuimarisha kipawa chake ili aweze kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**.
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**.
   Usawa wa kijamii kwa mfano usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa. Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zilizo na changamoto kwa mazoezi ya pamoja na ushirika katika huduma za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**.
   Elimu inafaa kutoa nafasi kwa wanaosoma kuelewa, kuthamini, kukuza na kudumisha tamaduni faafu na kudondoa zile potofu kulingana na jamii ya wakati uliopo ili kujenga jamii ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**.
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**.
   Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Elimu inafaa pia kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira. Inafaa kuwaelekeza vijana wa Kenya kukubali haja ya mazingira safi.

DRAFT

## MTAALA WA STASHAHADA YA UALIMU WA SHULE YA CHEKECHEA NA MSINGI

## KAULI KIINI

Kiswahili ni lugha ya taifa na rasmi nchini Kenya na somo la lazima katika elimu ya msingi. Wakenya wengi hujifunza lugha hii kama lugha ya pili. Hivyo, ni muhimu mkurufunzi kujifunza lugha ya Kiswahili. Hii itampa umilisi wa kumwezesha mwanafunzi kujenga stadi na umahiri ufaao wa kuwasiliana, kutangamana na kushiriki katika miktadha mbalimbali kwa kutumia lugha hii.

Mafunzo ya mbinu za kufundishia yanatarajiwa kumpa mkurufunzi umilisi, ujuzi na mtazamo chanya wa lugha ya Kiswahili ili kufanikisha shughuli za ujifunzaji. Mafunzo haya aidha yanatarajiwa kumhami kwa mbinu za kufundishia vipengele mbalimbali vya lugha. Vipengele hivi ni: Kusikiliza, Kuzungumza, Kusoma, Kuandika na Sarufi. Aidha, mafunzo haya yatamwandaa mkurufunzi kwa masomo ya viwango vya juu na kutekeleza majukumu yanayoambatana na taaluma ya ualimu.

## MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA MAFUNZO YA KISWAHILI YA STASHAHADA YA UALIMU WA SHULE YA CHEKECHEA NA MSINGI

Kufikia mwisho wa kozi ya Stashahada ya Ualimu wa Shule ya Msingi na chekechea, mkurufunzi aweze:

1. kutumia mbinu zifaazo kumwezesha mwanafunzi kupata umilisi unaotarajiwa wa somo la Kiswahili
2. kudhihirisha uwezo wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili ifaavyo katika mawasiliano na utangamano katika jamii
3. kuhakiki kazi mbalimbali za fasihi kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya kisanaa ili kumwezesha mwanafunzi kuandika kazi za kubuni za kiwango chake
4. kutumia vifaa vya kidijitali na nyenzo nyinginezo kufanikisha ujifunzaji
5. kudhihirisha ujuzi katika kuandaa na kutumia vitendeakazi vya taaluma ya ualimu kama vile azimio la kazi na andao la somo ili kufanikisha shughuli ya ujifunzaji

6. kutambua na kujumuisha shughuli za huduma za kijamii zinazochangia ujifunzaji, masuala mtambuko na maadili katika ujifunzaji
7. kutumia njia zifaazo za kutathmini kiwango cha umilisi wa mwanafunzi ili kufanikisha ujifunzaji
8. kudhihirisha uwezo wa kuzingatia elimu jumuishi katika mchakato wa ujifunzaji
9. kuthamini na kuonea fahari matumizi ya Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Historia ya Kiswahili** | **1.1.1 Chimbuko na Maenezi ya Kiswahili**<br><br>**(Saa 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kubainisha na kutathmini nadharia kuhusu chimbuko la Kiswahili Afrika Mashariki na Kati,<br>b) kujadili sababu za maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati,<br>c) kutambua na kujadili changamoto zilizokabili maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati,<br>d) kuhakiki ufaafu wa kauli kiini ya mtaala | Mkurufunzi aweze:<br>• kubainisha na kutathmini nadharia za chimbuko la Kiswahili *(Kiswahili kama lugha ya Kiarabu, ya mseto na ya Kibantu),*<br>• kushiriki katika mjadala kuhusu nadharia za chimbuko la Kiswahili *(mkurufunzi athibitishe msimamo wake kwa kuwasilisha mbele ya wenzake),*<br>• kutumia vifaa vya kidijitali kusakura maelezo kuhusu historia na maenezi ya Kiswahili,<br>• kuchora ramani inayoonyesha chimbuko na maenezi ya Kiswahili,<br>• kujadili sababu za maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika | Vyombo vya teknolojia, habari na mawasiliano vina mchango upi katika maenezi ya Kiswahili? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | wa somo la Kiswahili kwa mujibu wa maenezi ya Kiswahili,<br>e) kuchangamkia kuenea na kukua kwa Kiswahili katika Afrika Mashariki na Kati ili kukikuza. | Mashariki na Kati,<br>• kutambua na kujadili changamoto zilizokabili maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati, *(suala la mshikamano wa kitaifa*)<br>• kuhakiki ufaafu wa kauli kiini ya mtaala wa Somo la Kiswahili kwa kuzingatia maenezi ya Kiswahili. | |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhiriki na kuchangia katika mijadala na kazi za kikundi kuhusu historia na maenezi ya Kiswahili.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusakura ili kupata habari za kujifunzia historia na maendeleo ya Kiswahili.<br>• Uraia na uongozi – mkurufunzi anapochukua nyadhifa mbalimbali katika kikundi kujadili historia na maenezi ya Kiswahili nchini.<br>• Tathmini – mkurufunzi anapohakiki maoni ya wenzake katika mawasilisho. | | | | |
| **Maadili:**<br>• Umoja – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi.<br>• Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wengine wakati wanapojadiliana kuhusu nadharia za chimbuko la Kiswahili. | | | | |

DRAFT

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kubainisha na kutathmini nadharia kuhusu chimbuko la Kiswahili. | Anabainisha na kutathmini kwa mapana nadharia kuhusu chimbuko la Kiswahili. | Anabainisha na kutathmini nadharia kuhusu chimbuko la Kiswahili. | Anabainisha na kutathmini baadhi ya nadharia kuhusu chimbuko la Kiswahili. | Anabainisha bila kutathmini nadharia kuhusu chimbuko la Kiswahili. |
| Kujadili sababu za maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. | Anajadili sababu za maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati kwa uwazi na mtiririko bora. | Anajadili sababu za maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. | Anajadili baadhi ya sababu za maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. | Anataja bila kufafanua baadhi ya sababu za maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. |
| Kutambua na kujadili changamoto zilizokabili maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. | Anatambua na kujadili kwa kina changamoto zilizokabili maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. | Anatambua na kujadili changamoto zilizokabili maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. | Anajadili baadhi ya changamoto zilizokabili maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. | Anataja bila kujadili baadhi ya changamoto zilizokabili maenezi ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru katika Afrika Mashariki na Kati. |
| Kuhakiki ufaafu wa kauli kiini ya mtaala wa Somo la Kiswahili. | Anahakiki ufaafu wa kauli kiini ya mtaala wa Somo la Kiswahili kwa urahisi. | Anahakiki ufaafu wa kauli kiini ya mtaala wa Somo la Kiswahili ipasavyo. | Anahakiki ufaafu wa kauli kiini ya mtaala wa Somo la Kiswahili wa kwa kutoa hoja chache mno. | Anahakiki ufaafu wa kauli kiini ya mtaala wa Somo la Kiswahili kwa kutoa hoja chache mno na kwa usaidizi wa wenzake. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.2.1 Misingi ya Kusikiliza na Kuzungumza**<br><br>**(Saa 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili madhumuni ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza katika lugha,<br>b) kutambua na kutumia mikakati mwafaka ya kusikiliza na kuzungumza katika mawasiliano,<br>c) kujadili vikwazo vya kusikiliza na kuzungumza na utatuzi wake,<br>d) kuonea fahari stadi ya kusikiliza na kuzungumza | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili na wenzake madhumuni ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza shuleni,<br>• kutambua na kutumia mikakati mbalimbali ya kusikiliza na kuzungumza (*k.v. kuuliza maswali, kuzungumza kwa zamu, matumizi ya viziada lugha, kuzingatia sauti [kiimbo, shadda, kidatu], ufasiri, kusikiliza kwa makini*),<br>• kusikiliza na kutazama matumizi ya mikakati mbalimbali ya kusikiliza na kuzungumza kwa kutumia vifaa vya kidijitali,<br>• kuigiza mazungumzo akizingatia mikakati mbalimbali ya kusikiliza na kuzungumza,<br>• kutathmini ubora wa maigizo ya wenzake kwa heshima na upendo<br>• kujadili manufaa ya mikakati mbalimbali ya kusikiliza na kuzungumza, | Ni vipi tunaweza kuimarisha usikilizaji na uzungumzaji katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | katika maisha ya kila siku. | • kujadili vikwazo vya kusikiliza na kuzungumza,<br>• kupendekeza mikakati ya kutatua vikwazo vya kusikiliza na kuzungumza. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Tathmini – mkurufunzi anapotathmini ubora wa maigizo ya wenzake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mkurufunzi anapopendekeza mikakati ya kutatua vikwazo vya kusikiliza na kuzungumza.
- Uraia na uongozi – wakurufunzi wenye uwezo mbalimbali wanaposhirikishwa katika vikundi na kuigiza mazungumzo. wakizingatia mikakati mbalimbali ya kusikiliza na kuzungumza. Pia, mkurufunzi anapochukua nafasi mbalimbali za uongozi katika shughuli za vikundi.
- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza na kutazama matumizi ya mikakati mbalimbali ya kusikiliza na kuzungumza.
- Kujiamini – mkurufunzi anapoigiza ipasavyo mazungumzo akizingatia mikakati mbalimbali ya kusikiliza na kuzungumza.

**Maadili:**

- Umoja – mkurufunzi anaposhiriki katika mijadala.
- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wakati wa mijadala.
- Uwajibikaji – mkurufunzi anapochukua majukumu tofautitofauti katika maigizo.

DRAFT

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili madhumuni ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza. | Anajadili madhumuni ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza kwa ufasaha na wepesi. | Anajadili madhumuni ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza kwa ufasaha. | Anajadili baadhi ya madhumuni ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza. | Ana changamoto kujadili madhumuni ya kufundisha stadi ya kusikiliza na kuzungumza. |
| Kutambua na kutumia mikakati mwafaka ya kusikiliza na kuzungumza katika mawasiliano ipasavyo. | Anatambua na kutumia mikakati mwafaka ya kusikiliza na kuzungumza katika mawasiliano ipasavyo na kwa urahisi. | Anatambua na kutumia mikakati mwafaka ya kusikiliza na kuzungumza katika mawasiliano ipasavyo. | Anatambua na kutumia baadhi ya mikakati mwafaka ya kusikiliza na kuzungumza ipasavyo. | Anatambua baadhi ya mikakati ya kusikiliza na kuzungumza bila kuitumia ipasavyo katika mawasiliano. |
| Kujadili vikwazo vya kusikiliza na kuzungumza na utatuzi wake. | Anajadili kwa urahisi vikwazo vya kusikiliza na kuzungumza na utatuzi wake. | Anajadili vikwazo vya kusikiliza na kuzungumza na utatuzi wake. | Anajadili vikwazo vichache vya kusikiliza na kuzungumza na utatuzi wake. | Anajadili vikwazo vichache vya kusikiliza na kuzungumza bila kupendekeza utatuzi wake. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kusoma** | **1.3.1 Msingi wa Stadi ya Kusoma**<br><br>**(Saa 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili shabaha za kufundisha stadi ya kusoma shuleni ipasavyo,<br>b) kutambua na kueleza aina na namna mbalimbali za kusoma katika miktadha mbalimbali,<br>c) kusoma matini kwa kuzingatia namna mbalimbali za usomaji ili kufanikisha ujifunzaji,<br>d) kujadili matatizo ya usomaji na | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili shabaha za ufundishaji wa stadi ya kusoma,<br>• kutambua aina mbalimbali za kusoma (*kama vile: kusoma kwa ufahamu, kusoma kwa kina, kusoma kwa mapana, kusoma kwa kulenga dhana/wazo muhimu na upitiaji upesi*),<br>• kujadili namna mbalimbali za kusoma *(kusoma kimoyomoyo na kusoma kwa sauti),*<br>• kufanya mazoezi ya kusoma matini kwa kuzingatia aina mbalimbali za kusoma akitumia vifaa vya kidijitali na aina nyingine za matini,<br>• kufanya mazoezi ya kusoma matini kwa kuzingatia namna mbalimbali za kusoma akitumia vifaa vya kidijitali na aina nyingine za matini,<br>• kujadili na wenzake matatizo ya usomaji yanayowakumba wanafunzi (*k.v. Kusoma kwa kupindua silabi, athari ya lugha ya mama, kuruka maneno au sentensi, kubabaika bila makini, kusoma kwa* | Kusoma kuna umuhimu gani katika maisha ya kila siku? |



DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | utatuzi wake miongoni mwa wanafunzi,<br>e) kutambua na kutumia mbinu mbalimbali zinazotumiwa kujifunzia na kufunzia kusoma kwa watoto wa chekechea na shule ya msingi,<br>f) kuchangamkia nafasi ya usomaji katika mawasiliano. | *kutozingatia alama za uakifishaji, kugugumiza n.k.*),<br>• kujadili na wenzake jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wenye matatizo ya usomaji (*k.v. kumakinika, kuwahimiza wanafunzi, kuwapa wanafunzi mazingira huru ya kujifunzia, kuwajasirisha wanafunzi; maigizo na nyimbo, kuwapatia mazoezi ya kutamka sauti na kusoma*),<br>• kujadili na wenzake mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa kufundishia kusoma kwa watoto wa shule ya chekechea na ya msingi,<br>• kufanya mazoezi ya kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia kusoma kwa watoto wa shule ya chekechea nay a msingi,<br>• kufanya mradi wa kuchunguza matatizo ya usomaji miongoni mwa wanafunzi wa shule ya chekechea na ya msingi iliyo karibu na kuwasaidia kutatua matatizo yao ya usomaji akishirikiana na wenzake pamoja na walimu wa shule husika kwa kutumia mbinu alizojifunza. | |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Tathmini – mkurufunzi anapofanya mazoezi ya kusoma akiwa na wenzake.<br>• Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kutambua aina mbalimbali za kusoma. | | | | |

- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake kufanya mazoezi ya kusoma kwa kuzingatia aina mbalimbali za kusoma.
- Hamu ya ujifunzaji na utafakuri – mkurufunzi anapofanya mazoezi ya kusoma kwa kuzingatia aina mbalimbali za kusoma akitumia vifaa vya kidijitali na aina nyingine za matini.

**Maadili:**

- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni na mawasilisho ya wenzake.
- Uwajibikaji – mkurufunzi anapochukua majukumu mbalimbali katika mchakato wa ujifunzaji.
- Upendo – mkurufunzi anapotathmini mawasilisho ya wenzake kwa upendo.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarijio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili shabaha za kufundisha stadi ya kusoma ipasavyo. | Anajadili shabaha za kufundisha stadi ya kusoma ipasavyo na kwa wepesi. | Anajadili shabaha za kufundisha stadi ya kusoma ipasavyo. | Anajadili baadhi ya shabaha za kufundisha stadi ya kusoma ipasavyo. | Anajadili shabaha zisizo za kufundisha stadi ya kusoma. |
| Kutambua na kueleza aina na namna mbalimbali za kusoma. | Anatambua na kueleza aina na namna mbalimbali za kusoma kwa urahisi. | Anatambua na kueleza aina na namna mbalimbali za kusoma. | Anatambua na kueleza baadhi ya aina na namna za kusoma. | Anatambua lakini ana changamoto kueleza aina na namna mbalimbali za kusoma. |
| Kusoma matini kwa kuzingatia namna mbalimbali za | Anasoma matini kwa ufasaha kwa kuzingatia namna | Anasoma matini kwa kuzingatia namna mbalimbali | Anasoma matini kwa kuzingatia baadhi ya namna za usomaji. | Anasoma matini kwa kuzingatia baadhi ya namna za usomaji kwa |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| usomaji. | mbalimbali za usomaji. | za usomaji. | | kusaidiwa. |
| Kujadili matatizo ya usomaji na utatuzi wake. | Anajadili matatizo ya usomaji na utatuzi wake kikamilifu na kwa urahisi. | Anajadili matatizo ya usomaji na utatuzi wake. | Anajadili baadhi ya matatizo ya usomaji na utatuzi wake. | Anajadili baadhi ya matatizo ya usomaji bila kupendekeza utatuzi wake. |
| Kutambua na kutumia mbinu mbalimbali zinazotumiwa kujifunzia na kufunzia kusoma kwa wanafunzi wa chekechea na shule ya msingi. | Anatambua na kutumia mbinu mbalimbali zinazotumiwa kujifunzia na kufunzia kusoma kwa mwanafunzi chekechea na shule ya msingi. | Anatambua na kutumia mbinu mbalimbali zinazotumiwa kujifunzia na kufunzia kusoma kwa mwanafunzi wa chekechea na shule ya msingi. | Anatambua na kutumia baadhi ya mbinu mbalimbali zinazotumiwa kujifunzia na kufunzia kusoma kwa mwanafunzi wa chekechea na wa shule ya msingi. | Anatambua na kutumia baadhi ya mbinu mbalimbali zinazotumiwa kujifunzia na kufunzia kusoma kwa mwanafunzi wa chekechea na shule ya msingi |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo |
| --- | --- |
| **1.4 Kuandika** | **1.4.1 Misingi ya Stadi ya Kuandika**<br><br>**(Saa 2)** |

DRAFT

DRAFT

DRAFT

| | |
|---|---|
| | |

DRAFT

| | |
|---|---|
| | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – wakurufunzi wanaposhiriki katika kujadiliana kuhusu umuhimu wa stadi ya kuandika.
- Uraia na uongozi – wakurufunzi kutoka maeneo mbalimbali wanaposhirikishwa katika kazi za vikundi. Pia wanapochukua nafasi mb
- Tathmini – mkurufunzi anapotathmini matokeo maalum ya wenzake.

**Maadili:**

- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika mchakato wa ujifunzaji. Pia anapowatolea wenzake maoni kwa hesh
- Upendo – mkurufunzi anapowatolea wenzake maoni kwa upendo.
- Umoja – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana kuhusu maana na madhumuni ya kuandika.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili maana na umuhimu wa stadi ya kuandika. | Anajadili maana na umuhimu wa stadi ya kuandika kwa ubunifu wa hali ya juu. | Anajadili maana na umuhimu wa stadi ya kuandika. | Anajadili maana ya stadi ya kuandika na kutaja hoja chache kuhusu umuhimu wake. | Anajadili maana na umuhimu wa stadi ya kuandika kwa kusaidiwa. |
| Kuhusisha stadi ya kuandika na stadi zingine za lugha. | Anahusisha stadi ya kuandika na stadi zingine za lugha kwa usahihi na urahisi. | Anahusisha stadi ya kuandika na stadi zingine za lugha kwa usahihi. | Anahusisha stadi ya kuandika na baadhi ya stadi zingine za lugha kwa usahihi. | Anahusisha stadi ya kuandika na stadi zingine za lugha bila usahihi. |
| Kutambua na kujadili hatua za kimsingi za uandishi. | Anatambua na kujadili hatua za kimsingi za uandishi kikamilifu na kwa urahisi. | Anatambua na kujadili hatua za kimsingi za uandishi. | Anatambua na kujadili baadhi ya hatua za kimsingi za uandishi. | Anatambua hatua chache za kimsingi za uandishi lakini bila kuzijadili. |
| Kuandaa matokeo maalum ya kufundishia stadi ya kuandika kwa kuzingatia sifa za matokeo faafu. | Anaandaa kwa ubunifu matokeo maalum ya kufundishia stadi ya kuandika kwa kuzingatia sifa za matokeo faafu. | Anaandaa matokeo maalum ya kufundishia stadi ya kuandika kwa kuzingatia sifa za matokeo faafu. | Anaandaa matokeo maalum ya kufundishia stadi ya kuandika bila kuzingatia baadhi ya sifa za matokeo faafu. | Anaandaa matokeo maalum ya kufundishia stadi ya kuandika kwa kusaidiwa. |
| Kuandaa shughuli ya ujifunzaji kuhusu stadi ya kuandika kwa mwanafunzi wa shule ya chekechea na wa shule ya msingi. | Anaandaa shughuli ya ujifunzaji kuhusu stadi ya kuandika kwa mwanafunzi wa shule ya chekechea na wa shule ya msingi kwa wepesi. | Anaandaa shughuli ya ujifunzaji kuhusu stadi ya kuandika kwa mwanafunzi wa shule ya chekechea na wa shule ya | Anaandaa baadhi ya shughuli ya ujifunzaji kuhusu stadi ya kuandika kwa mwanafunzi wa shule ya chekechea na wa shule ya msingi. | Anaandaa baadhi ya shughuli ya ujifunzaji kuhusu stadi ya kuandika kwa mwanafunzi wa shule ya chekechea na wa |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | msingi. | | shule ya msingi. kwa kuelekezwa. |
| Kujadili jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wa shule ya chekechea wenye changamoto za kuandika, | Anajadili jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wa shule ya chekechea wenye changamoto za kuandika kwa wepesi. | Anajadili jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wa shule ya chekechea wenye changamoto za kuandika, | Anajadili jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wa shule ya chekechea wenye changamoto za kuandika, | Anajadili jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wa shule ya chekechea wenye changamoto za kuandika kwa kuelekezwa. |

DRAFT

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Swali Dadisi Lililopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Kuandika** | **1.4.2 Aina za Uandishi**<br><br>**(Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili na kulinganisha aina mbalimbali za uandishi katika matini mbalimbali,<br>b) kutambua aina mbalimbali za uandishi katika matini mbalimbali,<br>c) kuibua shughuli za ujifunzaji zinazoweza kufanikisha ufunzaji wa aina mbalimbali za uandishi,<br>d) kuonea fahari uandishi wa aina mbalimbali maishani. | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili aina mbalimbali za uandishi (*k.v: uandishi wa kiubunifu, uandishi wa kiuamilifu, uandishi wa kisanii, n.k),* | Unawezaje kutofautisha aina mbalimbali za uandishi katika lugha ya Kiswahili? |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | • kutoa mifano mwafaka kuonyesha uhusiano uliopo kati ya aina mbalimbali za uandishi,<br>• kusoma matini mbalimbali na kutambua maandishi ya kiubunifu, kiuamilifu na kisanii, | | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuibua shughuli za ujifunzaji zinazoweza kufanikisha ufunzaji wa aina mbalimbali za uandishi,<br>• kuwasilisha shughuli zake za ujifunzaji kwa wenzake ili kuzitathmini. | |

DRAFT

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Kujiamini – mkurufunzi anapotambua aina mbalimbali za uandishi.
- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadiliana kuhusu aina za uandishi.
- Uraia na uongozi – wakurufunzi wanaotoka katika maeneo mbalimbali wanaposhiriki katika kazi ya kikundi na kuchukua nafasi mbalimbali.

**Maadili:**

- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Umoja – mkurufunzi anaposhiriki katika kazi za kikundi kujadiliana kuhusu aina za uandishi.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili na kulinganisha aina mbalimbali za uandishi. | Anajadili na kulinganisha aina mbalimbali za uandishi kwa urahisi. | Anajadili na kulinganisha aina mbalimbali za uandishi. | Anajadili na kulinganisha baadhi ya aina za uandishi. | Anajadili baadhi ya aina za uandishi bila kuzilinganisha. |
| Kutambua aina mbalimbali za uandishi katika matini. | Anatambua kwa urahisi aina mbalimbali za uandishi katika matini. | Anatambua aina mbalimbali za uandishi katika matini. | Anatambua baadhi ya aina za uandishi katika matini. | Anatambua aina za uandishi katika matini kwa kusaidiwa. |
| Kuibua shughuli za ujifunzaji zinazoweza kufanikisha ufunzaji wa aina mbalimbali za uandishi. | Anaibua shughuli za ujifunzaji zinazoweza kufanikisha ufunzaji wa aina mbalimbali za uandishi kwa usahihi na ubunifu wa | Anaibua shughuli za ujifunzaji zinazoweza kufanikisha ufunzaji wa aina mbalimbali za uandishi kwa usahihi. | Anaibua baadhi ya shughuli za ujifunzaji zinazoweza kufanikisha ufunzaji wa aina mbalimbali | Anaibua shughuli chache za ujifunzaji zinazoweza kufanikisha ufunzaji wa aina mbalimbali za uandishi |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kiwango cha juu. | | za uandishi. | akisaidiwa na wenzake. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Kuandika** | **1.4.3 Kuandika Kidijitali (Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kufafanua maana na umuhimu wa uandishi wa kidijitali,<br>b) kuandika makala kwa kutumia vifaa vya kidijitali,<br>c) kuandaa shughuli zinazoweza kukuza umilisi wa ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi,<br>d) kuchangamkia uandishi wa kidijitali katika maisha ya kila siku. | Mkurufunzi aweze:<br>• kueleza maana ya kuandika kidijitali akiwa na wenzake,<br>• kujadili na wenzake kuhusu umuhimu wa uandishi wa kidijitali,<br>• kutumia vifaa vya kidijitali kuandika makala ya aina mbalimbali *(k.v. za insha ya kiubunifu na kiuamilifu),*<br>• kutumia wenzake makala yake kwa kutumia kifaa cha kidijitali, *(shirikisha masuala mtambuko anuwai*)<br>• kuhariri kazi za wenzake kwenye tarakilishi,<br>• kuandaa shughuli za ujifunzaji zinazowezesha ukuzaji wa umilisi wa ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi,<br>• kuwasilisha shughuli zake kwa wenzake ili kuzihakiki na kuzitolea maoni,<br>• kuhakiki shughuli za wenzake na kuwatolea maoni kwa upendo na heshima. | 1. Kuandika kidijitali kuna umuhimu gani?<br>2. Unazingatia nini unapoandika kwa kutumia kifaa vya kidijitali? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika uandishi.<br>• Mawasiliano na ushirikiano – wakurufunzi wanaposhirikishwa katika kujadili aina na umuhimu wa uandishi wa kidijitali.<br>• Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kutumia vifaa vya kidijitali katika uandishi.<br>• Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anapoandaa shughuli za ujifunzaji zinazowezesha ukuzaji wa ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi.<br>• Tathmini – mkurufunzi anapohakiki shughuli za ujifunzaji za wenzake. |
| --- |
| **Maadili:**<br>• Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi. Pia anapowatolea wenzake maoni kwa heshima.<br>• Upendo – mkurufunzi anapohakiki kazi za wenzake na kuwatolea maoni kwa upendo.<br>• Umoja – mkurufunzi anaposhiriki katika kazi za kikundi kueleza maana ya kuandika kidijitali na kujadiliana kuhusu umuhimu wake. |

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| Kufafanua maana na umuhimu wa uandishi wa kidijitali. | Anafafanua maana na umuhimu wa uandishi wa kidijitali ipasavyo na kwa ubunifu wa hali ya juu. | Anafafanua maana na umuhimu wa uandishi wa kidijitali ipasavyo. | Anafafanua maana na baadhi ya hoja kuhusu umuhimu wa uandishi wa kidijitali. | Anafafanua maana na baadhi ya hoja kuhusu umuhimu wa uandishi wa kidijitali akisaidiwa na wenzake. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuandika makala kwa kutumia vifaa vya kidijitali. | Anaandika makala kwa kutumia vifaa vya kidijitali kwa wepesi. | Anaandika makala kwa kutumia vifaa vya kidijitali. | Anaandika makala kwa kutumia vifaa vya kidijitali japo kwa kufanya makosa machache. | Anaandika makala kwa kutumia vifaa vya kidijitali akisaidiwa na wenzake. |
| Kuandaa shughuli zinazoweza kukuza umilisi wa ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi. | Anaandaa kwa urahisi shughuli zinazoweza kukuza umilisi wa ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi. | Anaandaa shughuli zinazoweza kukuza umilisi wa ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi. | Anaandaa shughuli chache zinazoweza kukuza umilisi wa ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi. | Anaandaa shughuli chache zinazoweza kukuza umilisi wa ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Kuandika** | **1.4.4 Ukuzaji wa Stadi ya Kuandika**<br><br>**(Saa 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili maana na umuhimu wa kuandika katika maisha ya kila siku,<br>b) kujadili hatua za ukuzaji wa stadi ya kuandika miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi na chekechea,<br>c) kujadili mbinu na kutambua mikakati inayotumiwa kufundishia kuandika katika shule za chekechea na za | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili umuhimu wa kuandika *(k.v kuwasiliana, kuweka rekodi, kuburudisha, kufahamisha na kuelimisha)*<br>• kujadili umuhimu wa kufunza dhana ya kuandika katika shule,<br>• kufanya mazoezi ya kuandika maumbo ya herufi, kuchora ruwaza, hati, neno, mafungu, imla,<br>• kujadili hatua za ukuzaji wa stadi ya kuandika *(k.v. kuandika msururu wa herufi, kuandika kwa kutofautisha herufi na maneno, kuanza kuendeleza maneno mepesi vizuri),*<br>• kujadili mbinu na mikakati ya kufundishia kuandika maumbo, ruwaza, hati na neno *(k.v. kuandika kwa kuwaonyesha; kuandika kwa pamoja; kuandika kwa kushirikiana; kuandika kwa kuelekezwa na kuandika pekee),* | 1. Stadi ya kuandika inahusianaje na stadi nyingine za lugha?<br>2. Unazingatia nini unapokuza stadi ya kuandika kwa wanafunzi wa shule ya chekechea? |



DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | msingi,<br>d) kuandaa shughuli za ujifunzaji kuhusu ukuzaji wa stadi ya kuandika,<br>e) kuchangamkia umuhimu wa stadi ya kuandika katika mawasiliano. | • kuandaa shughuli za ujifunzaji kuhusu ukuzaji wa stadi ya kuandika maumbo ya herufi, kuchora ruwaza, hati na neno katika shule ya chekechea na kuziwasilisha mbele ya wenzake,<br>• kutolea maoni shughuli za ujifunzaji za wenzake maoni,<br>• kujadili jinsi ya kuwasaidia wanafunzi wa shule ya chekechea walio na changamoto ya kuandika. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – wakurufunzi wanaposhirikishwa katika kujadiliana kuhusu umuhimu wa kuandika, hatua za uandishi, mbinu na mikakati ya kufundishia kuandika.
- Uraia na uongozi – wakurufunzi kutoka maeneo mbalimbali wanaposhirikisha katika mijadala mbalimbali. Pia wanapochukua nafasi mbalimbali za uongozi katika shughuli za mijadala.
- Tathmini – mkurufunzi anapohakiki shughuli za ujifunzaji za wenzake.
- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapofanya mazoezi ya kuandika maumbo ya herufi, kuchora ruwaza, hati, neno, mafungu, imla na ufupisho. Pia anapoandaa shughuli za ujifunzaji.

**Uhusiano na Maadili:**

- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika mchakato wa ujifunzaji. Pia anapowatolea wenzake maoni kwa heshima.
- Upendo – mkurufunzi anapowatolea wenzake maoni kwa upendo.
- Umoja – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana kuhusu uandishi.

DRAFT

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili maana na umuhimu wa kuandika. | Anajadili kwa ufasaha maana na umuhimu wa kuandika. | Anajadili maana na umuhimu wa kuandika. | Anajadili maana na baadhi ya sababu za kuandika. | Anatatizika kujadili maana na umuhimu wa kuandika. |
| Kujadili hatua za ukuzaji wa stadi ya kuandika. miongpni mwa wanafunzi wa shule ya chekechea na msingi. | Anajadili hatua za ukuzaji wa stadi ya kuandika miongoni mwa wanafunzi wa shule ya chekechea na msingi kwa urahisi. | Anajadili hatua za ukuzaji wa stadi ya kuandika miongoni mwa wanafunzi wa shule ya chekechea na msingi. | Anajadili baadhi ya hatua za ukuzaji wa stadi ya kuandika miongoni mwa wanafunzi wa shule wa chekechea na msingi. | Ana shida ya kujadili hatua za ukuzaji wa stadi ya kuandika miongoni mwa wanafunzi wa shule ya chekechea na msingi. |
| Kujadili mbinu na mikakati inayotumiwa kufundishia kuandika katika shule ya chekechea na ya msingi. | Anajadili kwa wepesi mbinu na mikakati inayotumiwa kufundishia kuandika katika shule ya chekechea na msingi. | Anajadili mbinu na mikakati inayotumiwa kufundishia kuandika katika shule ya chekechea na msingi. | Anajadili baadhi ya mbinu na mikakati inayotumiwa kufundishia kuandika katika shule ya chekechea na msingi. | Anajadili baadhi ya mbinu na mikakati inayotumiwa kufundishia kuandika katika shule ya chekechea na msingi kwa kusaidiwa. |
| Kuandaa shughuli za ujifunzaji kuhusu ukuzaji wa stadi ya kuandika wa chekechea na shule ya msingi. | Anaandaa shughuli za ujifunzaji kuhusu ukuzaji wa stadi ya kuandika wa chekechea na shule ya msingi. | Anaandaa shughuli za ujifunzaji kuhusu ukuzaji wa stadi ya kuandika wa chekechea na shule ya msingi. | Anaandaa shughuli za ujifunzaji kuhusu ukuzaji wa stadi ya kuandika wa chekechea na shule ya msingi akizingatia baadhi ya vipengele. | Ana changamoto kuandaa shughuli za ujifunzaji kuhusu ukuzaji wa stadi ya kuandika kwa shule ya chekechea na shule ya msingi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.5 Sarufi** | **1.5.1 Aina za Maneno**<br><br>**(Saa 6)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili dhana na umuhimu wa kufundisha sarufi shuleni,<br>b) kutambua na kutumia aina mahususi za maneno kwa ufasaha katika mawasiliano,<br>c) kujadili mbinu mwafaka za kufundishia aina za maneno katika lugha,<br>d) kuandaa maswali dadisi yanayoelekeza ujifunzaji wa aina za maneno, | Mkurufunzi aweze:<br>• kufanya utafiti maktabani na mtandaoni kuhusu dhana na umuhimu wa sarufi katika muktadha wa lugha ya Kiswahili,<br>• kujadili na kutoa mawasilisho darasani kuhusu umuhimu wa kufundisha sarufi katika shule ya msingi (*k.m. kujifunza kanuni za lugha, kufanikisha mawasiliano, kukuza stadi za kuandika na kuzungumza, kutambua utaratibu wa lugha ulivyo, kuongeza ujuzi wa lugha, kutumia lugha kwa ufasaha*),<br>• kutathmini mawasilisho ya wenzake kwa upendo na heshima,<br>• kujadili na wenzake aina mbalimbali za maneno (*Nomino, Viwakilishi, Vivumishi, Vitenzi, Vielezi, Vihusishi, Vihisishi, Viunganishi)* na migawanyo yake (*k.v. Nomino: za pekee, za kawaida, za dhahania*),<br>• kutambua aina mbalimbali za maneno katika kundi la maneno aliyopewa (*k.v. kwenye tarakilishi, mti maneno au kapu maneno*),<br>• kutunga sentensi sahihi kwa kutumia aina mbalimbali za maneno, | Ufunzaji wa sarufi una umuhimu gani kwa wanafunzi wa shule ya msingi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kuthamini ujifunzaji wa sarufi katika lugha ya Kiswahili. | • kujadili mbinu mbalimbali za kufundishia aina za maneno *(k.v. maswali na majibu, mkujadiliano, maigizo, maelezo)* akiwa na wenzake,<br>• kuandaa maswali dadisi yanayoweza kutumika katika ujifunzaji wa aina za maneno,<br>• kuwasilisha maswali dadisi aliyoandaa ili wenzake wamtolee maoni,<br>• kutathmini na kutoa maoni kuhusu maswali dadisi ya wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa :**

- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutafiti kuhusu dhana ya sarufi na umuhimu wa kufundisha sarufi shuleni.
- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhiriki na kuchangia katika mijadala kuhusu umuhimu wa kufundisha sarufi.
- Hamu ya ujifunzaji na utafakuri – mkurufunzi anapotafiti katika maktaba au mtandaoni kuhusu dhana ya sarufi.
- Tathmini – mkurufunzi anapowatolea wenzake maoni kuhusu mawasilisho yao.

**Maadili:**

- Uwajibikaji – mkurufunzi anapotafiti na kusakura katika tovuti salama. Pia anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kujadili kuhusu aina za maneno.
- Heshima – mkurufunzi anaposhiriki katika shughuli za vikundi huku akiheshimu na kuthamini maoni ya wenzake.

DRAFT

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili umuhimu wa kufundisha sarufi. | Anajadili umuhimu wa kufundisha sarufi kikamilifu na kwa wepesi. | Anajadili umuhimu wa kufundisha sarufi kikamilifu. | Anajadili baadhi ya hoja zinazohusu umuhimu wa kufundisha sarufi. | Anataja bila kujadili hoja chache zinazohusu umuhimu wa kufundisha sarufi. |
| Kutumia aina mahususi za maneno kwa ufasaha katika mawasiliano. | Anatumia aina mahususi za maneno kwa ufasaha na urahisi katika mawasiliano. | Anatumia aina mahususi za maneno kwa ufasaha katika mawasiliano. | Anatumia baadhi ya aina mahususi za maneno kwa ufasaha katika mawasiliano. | Anatumia aina chache mahususi za maneno katika mawasiliano kwa kuelekezwa. |
| Kujadili mbinu mwafaka za kufundishia aina za maneno. | Anajadili kwa urahisi mbinu mwafaka za kufundishia aina za maneno. | Anajadili mbinu mwafaka za kufundishia aina za maneno. | Anajadili baadhi ya mbinu mwafaka za kufundishia aina za maneno. | Anataja bila kujadili mbinu chache za kufundishia aina za maneno. |
| Kuandaa maswali dadisi yanayoelekeza ujifunzaji wa aina za maneno. | Anaandaa kwa wepesi maswali dadisi yanayoelekeza ujifunzaji wa aina za maneno. | Anaandaa maswali dadisi yanayoelekeza ujifunzaji wa aina za maneno. | Anaandaa maswali dadisi machache yanayoelekeza ujifunzaji wa aina za maneno. | Anaandaa maswali dadisi machache yanayoelekeza ujifunzaji wa aina za maneno kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma Kidijitali (Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili umuhimu wa usomaji kidijitali na sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali za | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili umuhimu na sifa za matini za kidijitali zinazofaa kusomwa na wanafunzi (*k.v. usalama mitandaoni, matini yenye lugha safi na sahihi, msamiati wa kiwango chake, maandishi yanayoonekana vyema, n.k)*<br>• kuhakiki matumizi ya nyenzo za kidijitali katika usomaji wa matini<br>• kujadili hatua za kiusalama katika usomaji wa matini za mtandaoni (*k.v. kufungua mitandao ifaayo, kutowasiliana na watu usiowajua, kutofichua nywila yako kwa wengine, n.k)*<br>• kutambua maadili yanayoendana na usomaji wa matini zilizohifadhiwa katika vifaa vya kidijitali *(k.v. kusoma matini zinazoruhusiwa, kutofuta kazi za wengine zilizohifadhiwa katika vifaa vya kidijitali)*<br>• kujadili umuhimu wa kuzingatia hatua za kiusalama na maadili katika usomaji wa kidijitali,<br>• kusoma matini mbalimbali ambazo zinashirikisha masuala mtambuko,<br>• kujadili na mwenzake kuhusu mikakati ya ufunzaji wa kusoma kidijitali,<br>• kuwawasilishia wenzake hatua za kiusalama na maadili aliyozingatia katika kusoma matini yake ya mtandaoni<br>• kusoma matini za kidijitali kwa kuzingatia maadili yafaayo<br>• kuandaa shughuli za usomaji zinazoelekea kukuza ujuzi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi<br>• kufanya mazoezi ya kufundisha akizingatia shughuli alizoziandaa na mikakati mwafaka ya ufunzaji wa kusoma kidijitali ili wenzake wamtolee maoni. | 1. Je, kusoma kidijitali kuna manufaa gani?<br>2. Unazingatia nini unaposoma matini za kidijitali? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kusomwa na wanafunzi,<br>b) kuhakiki matumizi ya nyenzo za kidijitali katika usomaji wa matini,<br>c) kusoma matini za kidijitali zinazoangazia masuala | | |

DRAFT

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mtambuko mbalimbali,<br>d) kutumia mikakati mwafaka ya ufunzaji wa kusoma kidijitali ili kukuza umilisi wa ujuzi wa kidijitali<br>e) kuchangamkia matumi | | | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | zi ya vifaa vya kidijitali katika kutafuta na kusoma matini ili kuimarisha maarifa yake. | | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusakura tovuti ili kutafuta matini lengwa na kuisoma kwa kuzingatia maadili.
- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake kutumia vifaa vya kidijitali kujifunza.
- Hamu ya ujifunzaji na utafakuri – mkurufunzi anaposakura mtandaoni ili kupata matini mbalimbali na kuzisoma akizingatia maadili katika usomaji wa kidijitali.
- Tathmini – mkurufunzi anapowatolea wenzake maoni kuhusu hatua za kisalama na maadili waliyazingatia katika usomaji wao.

**Maadili:**

- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kikundi. Pia anapowakosoa wenzake kwa heshima.
- Uwajibikaji – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kwa uwajibikaji na kuzingatia maadili.

DRAFT

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarijio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili umuhimu wa usomaji kidijitali na sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali. | Anajadili umuhimu wa usomaji kidijitali na sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali ipasavyo na kwa urahisi. | Anajadili umuhimu wa usomaji kidijitali na sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali ipasavyo. | Anajadili umuhimu wa usomaji kidijitali na baadhi ya sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali ipasavyo. | Anataja bila kujadili umuhimu wa usomaji kidijitali na baadhi ya sifa zinazozingatiwa kuteua matini za kidijitali. |
| Kuhakiki matumizi ya nyenzo za kidijitali. | Ankuhakiki matumizi ya nyenzo za kidijitali kwa ufasaha na wepesi. | Ankuhakiki matumizi ya nyenzo za kidijitali kwa ufasaha. | Ankuhakiki matumizi ya baadhi ya nyenzo za kidijitali. | Anahitaji usaidizi kuhakiki matumizi ya nyenzo za kidijitali. |
| Kutumia mikakati mwafaka ya ufunzaji wa kusoma kidijitali. | Anatumia mikakati mwafaka ya ufunzaji wa kusoma kidijitali ipasavyo na kwa urahisi. | Anatumia mikakati mwafaka ya ufunzaji wa kusoma kidijitali ipasavyo. | Anatumia baadhi ya mikakati mwafaka ya ufunzaji wa kusoma kidijitali. | Anatumia mikakati michache ya ufunzaji wa kusoma kidijitali kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Insha za Kiubunifu (Saa 5)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kubainisha insha za kiubunifu ili kuzitofautisha na insha nyingine,<br>b) kujadili aina za insha za kiubunifu ili kuzitambulisha,<br>c) kuandika insha za kiubunifu kwa maandishi ya hati na ya kidijitali,<br>d) kuandaa azimio la kazi la kufundishia aina mbalimbali za insha za kiubunifu katika Kiswahili,<br>e) kuandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kutumiwa kufunzia | Mkurufunzi aweze:<br>• kueleza maana ya insha za kiubunifu,<br>• kujadili aina za insha za kiubunifu (*k.v Mdokezo, Masimulizi, Maelezo, Picha, Methali, Mjadala na Wasifu*) kwa kuzitolea mifano,<br>• kutambua insha za kiubunifu katika matini au vifaa vya kidijitali,<br>• kuandika insha za kiubunifu kwa kutumia maandishi ya hati na vifaa vya kidijitali kama vile tarakilishi, (*shirikisha masuala mtambuko anuwai kama vile; masuala ya afya ya akili, elimu ya pesa, katika insha zinazoandikwa*)<br>• kuwasomae wenzake insha yake ili waitathmini,<br>• kuhakiki insha anazosomewa kwa ushirikiano na wenzake,<br>• kujadili mbinu mbalimbali za kufunzia insha za kiubunifu (*k.v. kutumia picha),*<br>• kuandaa azimio la kazi linaloweza kutumiwa kufundishia aina mbalimbali za insha za kiubunifu katika gredi za juu | Kuandika insha za kiubunifu kuna umuhimu gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | insha za kiubunifu katika Kiswahili<br>f) kutambua na kutumia mbinu mwafaka za kufundishia insha za kiubunifu<br>g) kuthamini uandishi wa aina mbalimbali za insha za Kiswahili. | za shule ya msingi,<br>• kupanga shughuli za ujifunzaji zinazoweza kutumiwa kufunzia insha za kiubunifu,<br>• kufanya mazoezi ya kufundisha insha za kiubunifu kwa kuzingatia azimio la kazi na mbinu mbalimbali,<br>• kujitathmini kuhusu ubora wa mbinu alizotumia katika mazoezi<br>• kutathmini wenzake kwa upendo na kuwatolea maoni kuhusu ubora wa mbinu walizozitumia katika mazoezi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Ubunifu na uvumbuzi - mkurufunzi anapobuni na kuandika insha akitumia mbinu zifaazo.
- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika insha.
- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapotambua na kutumia mbinu za kufundishia insha za kiubunifu.
- Tathmini – mkurufunzi anapohakiki insha za wenzake. Pia, anapojitathmini na kutathmini wenzake kuhusu ubora wa mbinu walizotumia katika mazoezi.

**Maadili:**

- Uwajibikaji – mkurufunzi anapojitathmini.
- Upendo – mkurufunzi anapowkutathmini wenzake.
- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake.
- Umoja – wakurufunzi wanaposhiriki katika kueleza maana na kujadiliana kuhusu mbinu za kufundishia insha za kiubunifu.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kubainisha insha za kiubunifu. | Anabainisha insha za kiubunifu kwa urahisi. | Anabainisha insha za kiubunifu. | Anabainisha baadhi ya insha za kiubunifu. | Anabainisha insha za kiubunifu kwa kusaidiwa. |
| Kujadili aina za insha za kiubunifu. | Anajadili aina za insha za kiubunifu kwa usahihi na wepesi. | Anajadili aina za insha za kiubunifu kwa usahihi. | Anajadili baadhi ya aina za insha za kiubunifu kwa usahihi. | Anataja bila kujadili baadhi ya aina za insha za kiubunifu. |
| Kuandika insha za kiubunifu kwa maandishi ya hati na ya kidijitali. | Anaandika kwa wepesi insha za kiubunifu kwa maandishi ya hati na ya kidijitali. | Anaandika insha za kiubunifu kwa maandishi ya hati na ya kidijitali. | Anaandika baadhi ya insha za kiubunifu kwa maandishi ya hati na ya kidijitali. | Anaandika baadhi ya insha za kiubunifu kwa maandishi ya hati na ya kidijitali kwa kusaidiwa. |
| Kuandaa azimio la kazi la kufundishia aina mbalimbali za insha za kiubunifu. | Anaandaa kwa wepesi azimio la kazi la kufundishia aina mbalimbali za insha za kiubunifu. | Anaandaa azimio la kazi la kufundishia aina mbalimbali za insha za kiubunifu. | Anaandaa azimio la kazi la kufundishia aina mbalimbali za insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya sehemu za azimio la kazi. | Anaandaa azimio la kazi la kufundishia baadhi ya insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya sehemu za azimio la kazi. |
| Kuandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kutumiwa kufunzia insha za kiubunifu | Anaandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kutumiwa kufunzia insha za kiubunifu | Anaandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kutumiwa kufunzia | Anaandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kutumiwa kufunzia insha za kiubunifu bila | Anaandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kutumiwa kufunzia insha za kiubunifu |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| katika Kiswahili | kikamilifu na kwa wepesi. | insha za kiubunifu kikamilifu. | kuzingatia mpangilio kamili. | kwa kuelekezwa. |
| Kutambua mbinu za kufundishia insha za kiubunifu. | Anatambua mbinu za kufundishia insha za kiubunifu kwa urahisi. | Anatambua mbinu za kufundishia insha za kiubunifu. | Anatambua baadhi ya mbinu za kufundishia insha za kiubunifu. | Anatambua mbinu chache za kufundishia insha za kiubunifu kwa kusaidiwa. |
| Kutumia mbinu za kufundishia insha za kiubunifu kwa usahihi. | Anatumia mbinu za kufundishia insha za kiubunifu kwa usahihi na wepesi. | Anatumia mbinu za kufundishia insha za kiubunifu kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya mbinu za kufundishia insha za kiubunifu kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya mbinu za kufundishia insha za kiubunifu bila usahihi. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1. Nyakati na Hali, Ukanushaji, Vinyume na Uambishaji (Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) Kutambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali kikamilifu katika sentensi za Kiswahili,<br>b) kukanusha sentensi za Kiswahili ipasavyo katika mawasiliano,<br>c) kutumia vinyume vya maneno katika sentensi za Kiswahili,<br>d) kutambua na kujadili aina mbalimbali za viambishi katika maneno ya Kiswahili,<br>e) kuandaa shughuli za ujifunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji | Mkurufunzi aweze:<br>• kutambua viambishi vya nyakati na hali mbalimbali kwenye sentensi zilizoandikwa kwenye chati, ubao au kifaa cha kidijitali k.v tarakilishi<br>• kutunga sentensi kwa kuzingatia nyakati na hali<br>• kueleza maana ya ukanushaji<br>• kukanusha sentensi mbalimbali za kiswahili<br>• kutambua vinyume vya maneno kwenye sentensi, chati, ubao au kifaa cha kidijitali k.v tarakilishi<br>• kutumia vinyume vya maneno katika sentensi<br>• kujadili aina mbalimbali za viambishi<br>• kutambua viambishi mbalimbali katika maneno<br>• kuwajibika kuandaa na kutumia nyenzo mwafaka za kufundishia nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji | Nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji huchangia vipi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | zinazoelekeza, ukuzaji wa maadili<br>f) kuandaa rekodi ya kazi kuhusu ufunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji katika Kiswahili,<br>g) kuchangamkia matumizi mwafaka ya nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na viambishi mbalimbali katika mawasiliano ya kila siku. | • kuandaa shughuli za kufundishia nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na viambishi mbalimbali zinayoonyesha jinsi ya kukuza maadili (*k.v. heshima, uwajibikaji, uadilifu, n.k*)<br>• kufanya mazoezi ya kufundisha nyakati na hali akizingatia shughuli alizoandaa na mbinu mwafaka za kufundishia ili wenzake wamtolee maoni<br>• kutathmini uwasilishaji wake na wa wenzake kwa upendo na heshima<br>• kuandaa rekodi ya kazi kuhusu ufunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapojifundisha na kutumia mbinu mwafaka za kufundishia dhana ya nyakati na hali.
- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotafiti kwenye mitandao kuhusu viambishi vya nyakati na hali na jinsi vinavyotumika katika lugha ya Kiswahili.
- Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anapoandaa na kutumia nyenzo mwafaka za kufundishia nyakati na hali. Pia, anapotumia chati, ubao au vifaa vya kidijitali kutambua viambishi vinavyobainisha nyakati na hali.
- Tathmini – mkurufunzi anapotathmini uwasilishaji wake na wa wenzake.
- Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kufundisha kwa kutumia mbinu zifaazo.

DRAFT

**Maadili:**

- Uwajibikaji – mkurufunzi anapotafiti kuhusu nyakati na hali maktabani na mtandaoni.
- Umoja, upendo na heshima – mkurufunzi anapothamini na kuheshimu mchango wa wenzake.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango<br>Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali kikamilifu katika sentensi za Kiswahili. | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali kikamilifu na kwa wepesi katika sentensi. | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali kikamilifu katika sentensi. | Anatambua na kutumia viambishi vichache vya nyakati na hali katika sentensi. | Anatambua na kutumia viambishi vichache vya nyakati na hali katika sentensi kwa kusaidiwa. |
| Kukanusha sentensi za Kiswahili kwa usahihi. | Anakanusha sentensi kwa usahihi na wepesi. | Anakanusha sentensi kwa usahihi. | Anakanusha baadhi ya sentensi kwa usahihi. | Anakanusha sentensi bila kuzingatia usahihi. |
| Kutumia vinyume vya maneno katika sentensi za Kiswahili. | Anatumia vinyume vya maneno katika sentensi kwa kwa usahihi na urahisi. | Anatumia vinyume vya maneno katika sentensi kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya vinyume vya maneno katika sentensi kwa usahihi. | Anatumia vinyume vya maneno katika sentensi bila usahihi. |
| Kutambua na kujadili aina mbalimbali za viambishi katika maneno ya Kiswahili. | Anatambua na kujadili aina mbalimbali za viambishi katika maneno ya Kiswahili | Anatambua na kujadili aina mbalimbali za viambishi katika maneno ya Kiswahili. | Anatambua na kujadili baadhi ya aina za viambishi katika maneno ya Kiswahili. | Anatambua bila kujadili baadhi ya aina za viambishi katika baadhi ya maneno ya Kiswahili. |



DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kwa wepesi. | | | |
| Kuandaa shughuli za ujifunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji zinazoelekeza ukuzaji wa maadili. | Anaandaa kwa ubunifu shughuli za ujifunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji zinazoelekeza ukuzaji wa maadili. | Anaandaa shughuli za ujifunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji zinazoelekeza ukuzaji wa maadili. | Anaandaa shughuli za ujifunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji zinazoelekeza ukuzaji wa baadhi ya maadili. | Anaandaa shughuli za ujifunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji zinazoelekeza ukuzaji wa baadhi ya maadili kwa kusaidiwa. |
| Kuandaa rekodi ya kazi kuhusu ufunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji. | Anaandaa rekodi ya kazi kuhusu ufunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji kikamilifu na kwa urahisi. | Anaandaa rekodi ya kazi kuhusu ufunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji kikamilifu. | Anaandaa rekodi ya kazi kuhusu ufunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya rekodi ya kazi. | Anaandaa rekodi ya kazi kuhusu ufunzaji wa nyakati na hali, ukanushaji, vinyume na uambishaji bila kuzingatia vipengele vyovyote. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.2. Matumizi ya 'kwa', 'ni', 'ki' na 'ji'**<br><br>**(Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kueleza matumizi ya ''kwa', 'ni', 'ki' na 'ji' katika lugha ya Kiswahili,<br>b) kutumia 'kwa', 'ni', 'ki' na 'ji' katika sentensi ipasavyo ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kuibua shughuli za ujifunzaji wa matumizi ya "kwa", "ni", "ki", "ji" na "na" zinazojumuisha masuala mtambuko,<br>d) kuonea fahari matumizi fasaha ya 'kwa', 'ni', 'na', 'ki' na 'ji' katika miktadha mbalimbali ya mawasiliano. | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili matumizi ya 'kwa', 'ni', 'ki' na 'ji' katika kikundi,<br>• kusakura katika mtandao maelezo na matumizi ya 'kwa', 'ni', 'ki' na 'ji' kwa uwajibikaji,<br>• kutunga sentensi sahihi kwa kutumia 'kwa', 'ni', 'ki' na 'ji',<br>• kutathmini sentensi zilizotungwa na wenzake na kuzitolea maoni kwa upendo na heshima kwa wenzake. *(Azingatie masuala mtambuko kuhusu elimu ya fedha*).<br>• kutoa muhtasari wa matumizi ya 'kwa', 'ni', 'ki' na 'ji' kwa kutumia mbinu anuwai (*k.v. matumizi ya chati, nyimbo, shairi au kifaa cha kidijitali*) na kuwasilishia wenzake,<br>• kuandaa shughuli za kufundishia zinazoonyesha jinsi ya kujumuisha masuala mtambuko kuhusu matumizi yafaayo ya vyombo vya usafiri katika ujifunzaji. | 'Kwa', 'ni', 'ki' na 'ji' hutekeleza majukumu gani katika lugha ya Kiswahili? |

DRAFT

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:** |
|---|
| • Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhiriki katika kazi ya kikundi na wenzake kubainisha matumizi sahihi ya ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’.<br>• Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapotafiti na kuwasilisha kazi yake darasani kuhusu matumizi ya ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji kwa kutumia mbinu anuwai (*k.v. matumizi ya chati, nyimbo, shairi au kifaa cha kidijitali*) na kuwasilishia wenzake.<br>• Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anaposhiriki katika ukuzaji na utumiaji wa nyenzo.<br>• Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kushiriki kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Maadili:** |
| • Uwajibikaji – mkurufunzi anapotafiti kuhusu matumizi sahihi ya ‘kwa’, ‘ni’, ‘na’, ‘ki’ na ‘ji’ maktabani na mtandaoni.<br>• Umoja na heshima – mkurufunzi anapotathmini kazi za wenzake kwa upendo na huku akiheshimu maoni na mchango wa wenzake. |

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza matumizi ya ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika lugha ya Kiswahili kwa usahihi. | Anaeleza matumizi ya ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika lugha ya Kiswahili kwa usahihi na ufasaha. | Anaeleza matumizi ya ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika lugha ya Kiswahili kwa usahihi. | Anaeleza baadhi ya matumizi ya ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika lugha ya Kiswahili kwa usahihi. | Anaeleza matumizi ya ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika lugha ya Kiswahili kwa kusaidiwa. |
| Kutumia ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika sentensi ipasavyo. | Anatumia ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika sentensi | Anatumia ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika sentensi | Anatumia ‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika baadhi ya | Anatumia ‘‘kwa’, ‘ni’, ‘ki’ na ‘ji’ katika sentensi kwa |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ipasavyo na kikamilifu. | ipasavyo. | sentensi ipasavyo. | kusaidiwa. |
| Kuibua shughuli za ujifunzaji wa matumizi ya “kwa”, “ni”, “ki”, “ji” na “na” zinazojumuisha masuala mtambuko. | Anaibua kwa urahisi shughuli za ujifunzaji wa matumizi ya “kwa”, “ni”, “ki”, “ji” na “na” zinazojumuisha masuala mtambuko. | Anaibua shughuli za ujifunzaji wa matumizi ya “kwa”, “ni”, “ki”, “ji” na “na” zinazojumuisha masuala mtambuko. | Anaibua shughuli za ujifunzaji wa matumizi ya “kwa”, “ni”, “ki”, “ji” na “na” zinazojumuisha baadhi ya masuala mtambuko. | Anaibua shughuli za ujifunzaji wa matumizi ya “kwa”, “ni”, “ki”, “ji” na “na” zinazojumuisha baadhi ya masuala mtambuko kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Sauti za Kiswahili**<br><br>**(Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kuainisha na kutamka irabu na konsonanti za lugha ya Kiswahili,<br>b) kujadi | Mkurufunzi aweze:<br>• kutambua na kujadili vigezo vinavyotumika katika kuainisha irabu na konsonanti,<br>• kujadili ala za kutamkia sauti mbalimbali za | 1. Shadda na kiimbo huwa na umuhimu gani katika mawasiliano?<br>2. Ni mikakati gani unayoweza kutumia kufundishia sauti za Kiswahili? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | li dhana za silabi, maneno, kiimbo na shadda katika lugha ya Kiswahili,<br>c) kutamka neno na sentensi ya Kiswahili kwa kuzingatia | lugha ya Kiswahili,<br>• kunukuu sauti za irabu na konsonanti kifonetiki,<br>• kutambua sauti inapotamkwa na mkufunzi, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>• kutamka na kunukuu sauti za irabu na konsona | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | shadda na kiimbo ipasavyo,<br>d) kuandaa maswali dadisi yanayolenga ujifunzaji wa sauti za Kiswahili,<br>e) kutambua na kutumia mikak | nti kifonetiki,<br>• kutambua sauti na jina la herufi,<br>• kusakura mtandao ili kupata bomba la sauti na kusoma maelezo yake,<br>• kutumia vifaa vya kidijitali kufundishia sauti,<br>• atamkie mwenzake neno na sentensi za | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ati ya kufundishia sauti za Kiswahili ili kuimarisha ujifunzaji,<br>f) kuhakiki ufaafu wa ujifunzaji wa kusikiliza na kuz | Kiswahili akizingatia shadda na kiimbo,<br>• kusikiliza na kutoa maoni kuhusu kazi ya mwezake,<br>• kuchora bomba la sauti na kutambulisha ala mbalimbali za matamshi,<br>• kushirikiana na wenzake | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ungumza kwa mujibu wa kauli kiini ya somo la Shughuli za Lugha katika shule za msingi na che | kujadili aina (*k.v. wazi na funge*) na miundo mbalimbali ya silabi (*k.v. KV, KKV, KKKV, K, V*),<br>• kutumia vifaa vya kidijitali kutambua aina na miundo mbalimbali ya silabi za Kiswahili.<br>• kutaja maneno | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kec hea,<br>g) kuthamini matamshi yafaayo ya sauti za Kiswahili katika mawasiliano. | kwa kuzingatia aina na miundo mbalimbali za silabi,<br>• kutamka neno na sentensi ya Kiswahili kwa kuzingatia shadda na kiimbo ipasavyo,<br>• kuandaa maswali dadisi yanayolenga ujifunzaj | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | i wa sauti za Kiswahili,<br>• kujadilia na katika vikundi kuhusu mikakati ya kufundishia sauti za Kiswahili (*k.v. kusikiliza sauti, kutamka katika kikundi, wawiliwawili na peke yake*)<br>• kufanya | |

DRAFT

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>mazoezi ya kutumia mbinu za kufundishia sauti za Kiswahili,<br>• kutathmini mawasilisho ya wenzake kwa upendo na heshima.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa<br>• Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kufundishia sauti. Pia, anapotumia vifaa vya kidijitali kusakura maelezo kuhusu uainishaji wa irabu na konsonanti za lugha ya Kiswahili.<br>• Mawasiliano na ushirikiano –mkurufunzi anaposhiriki katika mijadala darasani.<br>• Tathmini – kupitia tathmini inayofanywa na mkurufunzi katika mazoezi ya kufundisha darasani.<br>• Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kutamka maneno mbalimbali ifaavyo.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili<br>• Uwajibikaji – mkurufunzi anaposhiriki kufanya kazi mradi darasani. Pia, kupitia kushiriki katika kuandaa nyenzo na</td></tr>
</table>

| |
|---|
| kufanya mazoezi ya kufundishia darasani.<br>• Umoja – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake kafanya kazi kwa pamoja darasani. |

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kuainisha na kutamka irabu na konsonanti. | Anaainisha na kutamka irabu na konsonanti ipasavyo kwa ufasaha na wepesi. | Anaainisha na kutamka irabu na konsonanti ipasavyo. | Anaainisha na kutamka baadhi ya irabu na konsonanti ipasavyo. | Anaainisha na kutamka irabu na konsonanti kwa usaidizi wa wenzake. |
| Kujadili dhana za silabi, maneno, kiimbo na shadda. | Anajadili dhana za silabi, maneno, kiimbo na shadda kikamilifu na kwa ufasaha. | Anajadili dhana za silabi, maneno, kiimbo na shadda kikamilifu. | Anajadili dhana za silabi, maneno, kiimbo na shadda japo kwa kukosa ukamilifu. | Anajadili dhana za silabi, maneno, kiimbo na shadda kwa kuelekezwa. |
| Kutamka neno na sentensi ya Kiswahili kwa kuzingatia shadda na kiimbo ipasavyo. | Anatamka neno na sentensi ya Kiswahili kwa kuzingatia shadda na kiimbo ipasavyo na kwa urahisi. | Anatamka neno na sentensi ya Kiswahili kwa kuzingatia shadda na kiimbo ipasavyo. | Anatamka baadhi ya maneno na sentensi za Kiswahili kwa kuzingatia shadda na kiimbo. | Anatamka neno na sentensi ya Kiswahili kwa kuzingatia shadda na kiimbo akisaidiwa na wenzake. |
| Kuandaa maswali dadisi yanayolenga ujifunzaji wa sauti za Kiswahili | Anaandaa maswali dadisi yanayolenga ujifunzaji wa sauti za Kiswahili kikamilifu na kwa wepesi. | Anaandaa maswali dadisi yanayolenga ujifunzaji wa sauti za Kiswahili kikamilifu. | Anaandaa baadhi ya maswali dadisi yanayolenga ujifunzaji wa sauti za Kiswahili. | Anaandaa maswali dadisi finyu yanayolenga ujifunzaji wa sauti za Kiswahili. |
| Kutambua na | Anatambua na kutumia | Anatambua na | Anatambua na kutumia | Anatambua na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| kutumia mikakati ya kufundishia sauti za Kiswahili. | mikakati ya kufundishia sauti za Kiswahili kwa ufasaha na wepesi. | kutumia mikakati ya kufundishia sauti za Kiswahili kwa ufasaha. | baadhi ya mikakati ya kufundishia sauti za Kiswahili. | kutumia baadhi ya mikakati ya kufundishia sauti za Kiswahili kwa kusaidiwa. |
| Kuhakiki ufaafu wa ujifunzaji wa kusikiliza na kuzungumza kwa mujibu wa kauli kiini ya somo la Shughuli za Lugha katika shule za msingi na chekechea | Ankuhakiki ufaafu wa ujifunzaji wa kusikiliza na kuzungumza kwa mujibu wa kauli kiini ya somo la Shughuli za Lugha katika shule za msingi na chekechea kwa wepesi. | Ankuhakiki ufaafu wa ujifunzaji wa kusikiliza na kuzungumza kwa mujibu wa kauli kiini ya somo la Shughuli za Lugha katika shule za msingi na chekechea | Ankuhakiki kwa kiasi ufaafu wa ujifunzaji wa kusikiliza na kuzungumza kwa mujibu wa kauli kiini ya somo la Shughuli za Lugha katika shule za msingi na chekechea. | Ankuhakiki kwa kiasi ufaafu wa ujifunzaji wa kusikiliza na kuzungumza kwa mujibu wa kauli kiini ya somo la Shughuli za Lugha katika shule za msingi na chekechea kwa kusaidiwa. |

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Misingi ya Fasihi ya Watoto (Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili maana na dhima ya fasihi ya watoto katika jamii,<br>b) kujadili sifa za fasihi ya watoto ili kuweza kuteua | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili maana na dhima ya fasihi ya watoto (*kama vile kuburudisha, kuelimisha, kufahamisha na kuadilisha*)<br>• kujadili sifa za fasihi ya watoto huku akishirikiana na wenzake (*kama vile:* | 1. Ni mambo gani yanayotambulisha fasihi ya watoto?<br>2. Fasihi ya watoto ina umuhimu gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | vitabu vifaavyo vya hadithi,<br>c) kutambua aina za fasihi ya watoto katika jamii,<br>d) kuteua na kupendekeza vitabu vya fasihi ya watoto wa viwango mbalimbali katika kundi la vitabu vya hadithi<br>e) kuibua na kutumia nyenzo faafu kufundishia fasihi ya watoto<br>f) kuthamini fasihi ya watoto katika jamii. | *wahusika watoto, wahusika wanyama, picha zenye rangi, lugha nyepesi na maudhui yanayolingana na kiwango cha mtoto n.k*)<br>• kujadili aina za fasihi ya watoto (*k.v. hadithi za watoto, maigizo ya watoto, mashairi ya watoto, vibonzo vya watoto, n.k*) akiwa na wenzake<br>• kuteua vitabu vya aina mbalimbali vya watoto wa viwango mbalimbali (*k.v. katika maktabani au katika duka la vitabu*)<br>• kuigiza mambo aliyojifunza kutokana na vitau alivyosoma<br>• kupendekeza vitabu vinavyofaa watoto wa umri mbalimbali akizingatia masuala mtambuko,<br>• kuibua na kutumia nyenzo faafu kufundishia fasihi ya watoto. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhiriki katika mjadala pamoja na wenzake.
- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapoweza kuamua namna ya kuteua vitabu vifaavyo kulingana na sifa za fasihi ya watoto.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mkurufunzi anapoamua vitabu vinavyofaa kusomwa na watoto wenye uwezo wa kusoma wa viwango mbalimbali.
- Tathmini – mkurufunzi anapoweza kuamua na kuteua vitabu vifaavyo vya fasihi ya watoto.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Umoja – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake katika mijadala.<br>• Uwajibikaji – mkurufunzi anapoteua vitabu vya watoto kulingana na sifa bainifu. |

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarijio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili maana na dhima ya fasihi ya watoto. | Anajadili maana na dhima ya fasihi ya watoto ipasavyo na kwa urahisi. | Anajadili maana na dhima ya fasihi ya watoto ipasavyo. | Anajadili maana na baadhi ya dhima za fasihi ya watoto. | Anajadili maana na dhima ya fasihi ya watoto kwa kusaidiwa. |
| Kujadili sifa za fasihi ya watoto na kuteua vitabu vifaavyo vya hadithi. | Anajadili kikamilifu na kwa wepesi sifa za fasihi ya watoto na kuteua vitabu vifaavyo vya hadithi. | Anajadili kikamilifu sifa za fasihi ya watoto na kuteua vitabu vifaavyo vya hadithi. | Anajadili baadhi ya sifa za fasihi ya watoto na kuteua vitabu vifaavyo vya hadithi. | Anajadili sifa za fasihi ya watoto na kuteua vitabu vifaavyo vya hadithi akisaidiwa na wenzake. |
| Kutambua aina za fasihi ya watoto. | Anatambua aina za fasihi ya watoto kikamilifu na kwa urahisi. | Anatambua aina za fasihi ya watoto kikamilifu. | Anatambua baadhi ya aina za fasihi ya watoto. | Anatambua aina za fasihi ya watoto kwa msaada wa wenzake. |
| Kuteua na kupendekeza vitabu vya fasihi ya watoto wa viwango mbalimbali. | Ankuteuaa na kupendekeza vitabu vya fasihi ya watoto wa viwango mbalimbali ipasavyo na kwa wepesi. | Ankuteuaa na kupendekeza vitabu vya fasihi ya watoto wa viwango mbalimbali ipasavyo. | Ankuteuaa na kupendekeza baadhi ya vitabu vya fasihi ya watoto wa viwango mbalimbali. | Ankuteuaa na kupendekeza vitabu vya fasihi ya watoto wa viwango mbalimbali kwa kusaidiwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kuibua na kutumia nyenzo faafu kufundishia fasihi ya watoto. | Anaibua na kutumia nyenzo faafu kufundishia fasihi ya watoto ipasavyo na kwa urahisi. | Anaibua na kutumia nyenzo faafu kufundishia fasihi ya watoto ipasavyo. | Anaibua na kutumia baadhi ya nyenzo faafu kufundishia fasihi ya watoto. | Anaibua na kutumia nyenzo faafu kufundishia fasihi ya watoto kwa usaidizi wa wenzake. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.2 Uchambuzi wa Vitabu vya Fasihi ya Watoto (Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kutambua na kujadili vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto,<br>b) kusoma na kuchambua vitabu vya fasihi ya watoto ili kubainisha maudhui na fani<br>c) kuandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kukuza maadili, miongoni mwa watoto kupitia fasihi ya watoto<br>d) kuonea fahari nafasi ya fasihi ya watoto katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. | Mkurufunzi aweze:<br>• kutambua na kujadili vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto *(k.v. maudhui, fani mbalimbali n.k)*<br>• kusoma na kuchambua vitabu mbalimbali vya fasihi ya watoto vilivyoteuliwa na mkufunzi *(k.v vitabu vya hadithi, maigizo, mashairi, vibonzo, n.k)* kwa kuzingatia maudhui, fani na maadili yanayopitishwa kwa watoto ***(Mkufunzi kuteua vitabu vya fasihi ya watoto kwa kuzingatia viwango vya wanafunzi wa shule ya msingi),***<br>• kuteua vitabu vinavyozingatia masuala mtambuko anuia,<br>• kuandaa shughuli za ujifunzaji zinazoonyesha uwezo wa kukuza maadili mbalimbali *(k.v. umoja, amani upendo, haki za kijamii, uzalendo na uadilifu)* miongoni mwa wanafunzi kutokana na hadithi alizosoma, | Ni mambo gani hufunzwa watoto kupitia maudhui ya hadithi za watoto? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuandaa shughuli za ujifunzaji zinazozingatia ukuzaji wa maadili. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anaposoma na kuchambua hadithi.
- Tathmini – mkurufunzi anapotathmini hoja za wenzake katika kikundi kuhusu uchambuzi wa maudhui na fani.
- Uraia na uongozi – mkurufunzi anapochukua majukumu katika vikundi.
- Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kusoma na kuchambua hadithi.

**Maadili:**
- Uadilifu – mkurufunzi anapochambua vitabu vyenye maudhui yanayokuza maadili.
- Uwajibikaji – mkurufunzi anaposoma na kutunza vitabu anavyotumia vya hadithi.
- Upendo – mkurufunzi wanapotangamana na wenzake katika kikundi.
- Umoja – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake darasani.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarijio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kujadili vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto. | Anatambua na kujadili kwa urahisi vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto. | Anatambua na kujadili vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto. | Anatambua na kujadili baadhi ya vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto. | Anatambua lakini anatatizika kujadili vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa vitabu vya fasihi ya watoto. |
| Kusoma vitabu vya hadithi za watoto. | Anasoma hadithi za watoto kwa ufasaha na kwa wepesi. | Anasoma hadithi za watoto kwa ufasaha. | Anasoma hadithi za watoto bila ufasaha. | Anasoma baadhi ya hadithi za watoto kwa kusaidiwa. |
| Kusoma na | Anasoma na | Anasoma na | Anasoma na | Anasoma na |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| kuchambua vitabu vya fasihi ya watoto ili kujadili maudhui na fani. | kuchambua vitabu vya fasihi ya watoto na kujadili maudhui na fani kwa urahisi. | kuchambua vitabu vya fasihi ya watoto na kujadili maudhui na fani. | kuchambua vitabu vya fasihi ya watoto na kujadili baadhi ya maudhui na fani. | kuchambua vitabu vya fasihi ya watoto na kutaja baadhi ya maudhui na fani bila kujadili. |
| Kuandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kukuza maadili miongoni mwa watoto. | Anaandaa kwa ubunifu mkubwa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kukuza maadili miongoni mwa watoto. | Anaandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kukuza maadili miongoni mwa watoto. | Anaandaa shughuli za ujifunzaji zinazoweza kukuza baadhi ya maadili miongoni mwa watoto. | Anaandaa shughuli chache sana za ujifunzaji zinazoweza kukuza baadhi ya maadili miongoni mwa watoto. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llilopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Insha za Kiubunifu (Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kutambua na kujadili aina za insha za kiubunifu katika somo la Kiswahili,<br>b) kuandika insha za kiubunifu kwa kuzingatia vigezo muhimu vya uandishi wa insha katika somo la Kiswahili,<br>c) kutambua na kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia uandishi wa insha za kiubunifu katika Kiswahili,<br>d) kuthamini uandishi | Mkurufunzi aweze:<br>• kueleza maana ya insha za kiubunifu,<br>• kujadili aina za insha za kiubunifu kwa kuzitolea mifano (*k.v. mdokezo, masimulizi, maelezo, picha, methali, mjadala, wasifu*),<br>• kutambua insha za kiuamilifu katika matini au vifaa vya kidijitali,<br>• kuandika insha za kiubunifu kwa kuzingatia vigezo muhimu vya uandishi wa insha katika somo la Kiswahili (*k.v. maudhui, mtindo, sarufi, msamiati),*<br>• kuandika insha za kiubunifu kwa kutumia maandishi ya hati na vifaa vya kidijitali (*k.v. tarakilishi*) na kuwkusomaa wenzake insha yake,<br>• kuhakiki insha anazosomewa kwa ushirikiano na wenzake,<br>• kujadili mbinu mbalimbali za kufunzia insha za kiubunifu (*k.v. kutumia picha),*<br>• kufanya mazoezi ya kufundisha insha za kiubunifu kwa kuzingatia mbinu mbalimbali, | Insha za kiubunifu zinachangia vipi katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | wa aina mbalimbali za insha katika mawasiliano. | • kujitathmini kuhusu ubora wa mbinu alizotumia katika mazoezi<br>• kutathmini wenzake kwa upendo na kuwatolea maoni kuhusu ubora wa mbinu walizozitumia katika mazoezi<br>• kuonyesha uhusiano wa uandishi wa insha za kiubunifu na masomo mengine katika mtaala. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anapobuni na kuandika insha kwa kuzingatia vigezo muhimu vya uandishi wa insha.
- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika insha.
- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anapojadili aina za insha za kiubunifu na wenzake.
- Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kuandika insha ya kubuni ifaavyo.
- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapotambua na kutumia mbinu za kufundishia insha za kiubunifu
- Tathmini – mkurufunzi anapohakiki insha za wenzake. Pia, anapojitathmini na kutathmini wenzake kuhusu ubora wa mbinu walizotumia katika mazoezi.

**Maadili:**

- Upendo – mkurufunzi anapowkutathmini wenzake na kuwatolea maoni kwa upendo.
- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake.
- Umoja – mkurufunzi anaposhiriki katika kueleza maana na kujadiliana kuhusu mbinu za kufundishia insha za kiubunifu.

DRAFT

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kujadili aina za insha za kiubunifu. | Anatambua na kujadili aina za insha za kiubunifu kikamilifu. | Anatambua na kujadili aina za insha za kiubunifu. | Anatambua lakini ana shida ya kujadili baadhi ya aina za insha za kiubunifu. | Anatambua pasina kujadili aina za insha za kiubunifu kikamilifu. |
| Kuandika insha za kiubunifu kwa kuzingatia vigezo muhimu vya uandishi wa insha. | Anaandika insha za kiubunifu kwa kuzingatia vigezo muhimu ipasavyo na kwa ubunifu wa hali ya juu. | Anaandika insha za kiubunifu kwa kuzingatia vigezo muhimu ipasavyo. | Anaandika insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya vigezo muhimu. | Anaandika insha za kiubunifu lakini bila kuzingatia vigezo muhimu. |
| Kutambua na kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia insha za kiubunifu. | Anatambua na kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia insha za kiubunifu kwa ufasaha na urahisi. | Anatambua na kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia insha za kiubunifu kwa ufasaha. | Anatambua baadhi ya mbinu za kufundishia insha za kiubunifu bila kuzitumia. | Anatambua na kutumia baadhi ya mbinu za kufundishia insha za kiubunifu kwa msaada wa wenzake au mkufunzi. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Aina za Sentensi**<br><br>**(Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na cha uamilifu,<br>b) kuunda aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu ili kukuza umilisi wa ubunifu,<br>c) kuonea fahari matumizi fasaha ya sentensi za aina mbalimbali katika mawasiliano ya kila siku. | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadiliana na wenzake aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo (*k.v*: *sahili, ambatano na changamano),*<br>• kujadiliana na wenzake aina za sentensi kwa mujibu wa kigezo cha uamilifu (*k.v. ulizi, kauli, hisishi, amrishi na ombi),*<br>• kutambua aina mbalimbali za sentensi katika matini,<br>• kutunga sentensi za aina mbalimbali kwa kuzingatia kigezo cha muundo na kuziandika kwenye daftari au tarakilishi,<br>• kutunga sentensi za aina mbalimbali kwa kuzingatia kigezo cha uamilifu na kuziandika kwenye daftari au tarakilishi,<br>• kuwasilisha aina za sentensi alizotunga kwenye ubao, kwa kutumia chati au kifaa cha kidijitali,<br>• kutathmini sentensi alizotunga na wenzake kwa upendo na heshima,<br>• kuzibadilisha sentensi kwa mujibu wa maagizo aliyopewa ili kubainisha utendakazi. | Matumizi ya sentensi za aina mbalimbali yana umuhimu gani katika mawasiliano? |

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:** |
|---|
| • Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapotafiti kuhusu aina mbalimbali za sentensi maktabani na mitandaoni.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia tarakilishi ifaavyo kuwasilisha sentensi alizotunga.<br>• Uraia na uongozi – wakurufunzi walio na uwezo tofauti wanapotagusana katika shughuli za vikundi.<br>• Tathmini – wakurufunzi wanapotoleana maoni kuhusu sentensi zao. |
| **Maadili:**<br>Amani na umoja – Mkurufunzi anaposhirikiana na wengine katika kazi za vikundi. |

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na cha uamilifu. | Anajadili kwa wepesi aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu. | Anajadili aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na cha uamilifu. | Anajadili baadhi ya aina za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu. | Anajadili baadhi ya aina za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu kwa kusaidiwa. |
| Kuunda aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu ili kukuza umilisi wa ubunifu. | Anaunda kwa urahisi aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu. | Anaunda aina mbalimbali za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu. | Anaunda sentensi chache kwa kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu. | Anaunda sentensi chache bila kuzingatia kigezo cha muundo na uamilifu. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.2 Virai na Vishazi**<br><br>**(Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kueleza tofauti kati ya kirai na kishazi katika lugha ya Kiswahili,<br>b) kujadili na kuchanganua aina za virai na vishazi katika tungo za Kiswahili,<br>c) kutumia virai na vishazi ipasavyo kutunga sentensi za Kiswahili,<br>d) Kuchangamkia nafasi ya virai na vishazi katika tungo za Kiswahili. | Mkurufunzi aweze:<br>• kueleza maana ya kirai na ya kishazi,<br>• kueleza tofauti kati ya kirai na kishazi,<br>• kutafiti mitandaoni na maktabani kuhusu virai na vishazi,<br>• kujadili na kuchanganua aina za virai na vishazi akiwa na wenzake,<br>• kutumia virai ipasavyo kutunga sentensi za Kiswahili,<br>• kuchanganua kwenye vikundi aina za vishazi katika tungo za lugha ya Kiswahili,<br>• kutumia vishazi ipasavyo kutunga sentensi za Kiswahili. | 1. Kirai na kishazi hutofautiana vipi?<br>2. Ni nini dhima ya kirai na kishazi katika tungo? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kueleza tofauti iliyopo baina ya kirai na kishazi.
- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotafiti kuhusu virai na vishazi mtandaoni.
- Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anapotumia virai na vishazi ipasavyo kutunga sentensi.

**Uhusiano na Maadili:**

- Uwajibikaji – mkurufunzi anapotafiti kuhusu virai na vishazi maktabani na mtandaoni.

DRAFT

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza tofauti kati ya kirai na kishazi katika lugha ya Kiswahili. | Anaeleza tofauti kati ya kirai na kishazi kwa ukamilifu na wepesi. | Anaeleza tofauti kati ya kirai na kishazi kwa ukamilifu. | Anaeleza tofauti kati ya kirai na kishazi japo si kwa ukamilifu. | Anaeleza tofauti kati ya kirai na kishazi kwa kusaidiwa. |
| Kubainisha virai na vishazi katika tungo za Kiswahili. | Anabainisha kwa urahisi na wepesi virai na vishazi katika tungo za Kiswahili. | Anabainisha virai na vishazi kwa urahisi katika tungo za Kiswahili. | Anabainisha baadhi ya virai na vishazi katika tungo za Kiswahili. | Ana changamoto kubainisha virai na vishazi katika tungo za Kiswahili. |
| Kutumia virai na vishazi ipasavyo kutunga sentensi za Kiswahili. | Anatumia virai na vishazi ipasavyo na kwa urahisi kutunga sentensi za Kiswahili. | Anatumia virai na vishazi ipasavyo kutunga sentensi za Kiswahili. | Anatumia baadhi ya virai na vishazi ipasavyo kutunga sentensi za Kiswahili. | Anatumia virai na vishazi kutunga sentensi za Kiswahili kwa usaidizi wa wenzake. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.3 Uakifishaji (Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili dhana ya uakifishaji katika lugha ya Kiswahili,<br>b) kutumia alama mbalimbali za uakifishaji katika tungo za Kiswahili ili kuimarisha mawasiliano,<br>c) kutumia mbinu na mikakati mwafaka ya kufundishia uakifishaji,<br>d) kuthamini uakifishaji mwafaka katika tungo za Kiswahili ili kufanikisha mawasiliano. | Mkurufunzi aweze:<br>• kueleza maana ya uakifishaji,<br>• kujadili alama mbalimbali za uakifishaji,<br>• kutambua alama za uakifishaji katika matini mbalimbali,<br>• kutumia | Je, alama za uakifishaji katika lugha ya Kiswahili hutekeleza wajibu upi? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | alama mbalimbali za uakifishaji katika tungo za Kiswahili,<br>• kutafiti kuhusu mbinu zifaazo za kufundishia uakifishaji maktabani na mtandaoni,<br>• kubainisha mbinu mwafaka za kufundishia | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | uakifishaji, (*k.m* : *kuonyesha, maswali na majibu, mkujadiliano, maigizo* na *maelezo,*<br>• kuandaa shughuli za ujifunzaji zinazohusu uakifishaji zinazoweza kukuza umilisi wa mawasiliano na | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ushirikiano,<br>• kuandaa nyenzo zifaazo kufundishia shughuli za uakifishaji alizoziandaa (*kama vile chati, kadi maneno, matumizi ya vifaa vya kidijitali, n.k.*),<br>• kutumia mbinu na mikakati mwafaka | |

DRAFT

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | ya kufundishia shughuli alizozianda na kuwasilishia wenzake ili kuzitathmini,<br>• kutathmini mawasilisho ya wenzake kuhusu mazoezi ya kufundishia uakifishaji. | |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anaposhiriki katika mchakato wa kufundishia shughuli za uakifishaji akitumia | | | | | |

DRAFT

mbinu na mikakati mbalimbali.

- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu alama za uakifishaji. Pia, anapotafiti kuhusu mbinu na mikakati ya kufundishia uakifishaji katika lugha ya Kiswahili.
- Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anapoandaa shughuli za ujifunzaji zinazohusu uakifishaji na nyenzo zifaazo kufundishia uakifishaji.
- Kujiamini – mkurufunzi anaposhiriki kikamilifu katika mchakato wa ujifunzaji darasani. Haiba ya mkurufunzi inakuzwa anapowasilisha mbele ya wenzake.

**Maadili:**

- Uwajibikaji – mkurufunzi anapotafiti kuhusu uakifishaji maktabani na mtandaoni. Pia anaposhiriki katika shughuli za vikundi.
- Umoja na heshima – mkurufunzi anaposhiriki kikamilifu katika shughuli za vikundi huku akiheshimu na kuthamini maoni na mchango wa wenzake.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maana ya uakifishaji katika lugha za Kiswahili. | Anaeleza maana ya uakifishaji katika lugha za Kiswahili kwa ufasaha na wepesi. | Anaeleza maana ya uakifishaji katika lugha za Kiswahili kwa ufasaha. | Anaeleza kwa kutoa maelezo yasiyo kamilifu kuhusu uakifishaji katika lugha ya Kiswahili. | Anaeleza maana ya uakifishaji katika lugha ya Kiswahili kwa kusaidiwa. |
| Kutumia alama mbalimbali za uakifishaji katika tungo za Kiswahili. | Anatumia alama mbalimbali za uakifishaji katika tungo za Kiswahili kwa usahihi na | Anatumia alama mbalimbali za uakifishaji katika tungo za Kiswahili kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya alama za uakifishaji katika tungo za Kiswahili kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya alama za uakifishaji katika tungo za Kiswahili kwa usahihi kwa usaidizi wa |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | wepesi. | | | wenzake. |
| Kutumia mbinu na mikakati mwafaka ya kufundishia uakifishaji ili kuimarisha mawasiliano. | Anatumia mbinu na mikakati mwafaka ya kufundishia uakifishaji kwa usahihi na wepesi. | Anatumia mbinu na mikakati mwafaka ya kufundishia uakifishaji kwa usahihi. | Anatumia baadhi ya mbinu na mikakati mwafaka ya kufundishia uakifishaji. | Anatumia mbinu na mikakati yoyote ya kufundishia uakifishaji kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Isimujamii (Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kueleza dhana ya isimujamii ili kuitambulisha,<br>b) kutambua na kujadili majukumu mbalimbali ya lugha katika jamii,<br>c) kuigiza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya kijamii,<br>d) kufafanua sifa za sajili mbalimbali za lugha,<br>e) kuhakiki matini za Kiswahili kwa kubainisha sajili husika,<br>f) kutumia sajili mbalimbali za lugha katika miktadha tofauti ya kijamii<br>g) kutunga maswali dadisi yanayolenga ujifunzaji wa sajili za lugha katika jamii,<br>h) kuonea fahari matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali. | Mkurufunzi aweze:<br>• kueleza dhana ya isimujamii,<br>• kujadili majukumu mbalimbali ya lugha katika jamii (*k.v. lugha ya taifa, lugha ya kimataifa, lugha* | Kuna uhusiano gani kati ya lugha na jamii? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *rasmi, lingua franka, pijini, krioli na lafudhi*),<br>• kujadili matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali katika jamii (*k.v. muktadha rasmi na usio rasmi*),<br>• kuigiza matumizi yafaayo | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ya lugha katika miktadha mbalimbali (*miktadha rasmi na isiyo rasmi*),<br>• kutumia vifaa vya kidijitali katika kutafuta maelezo zaidi kuhusu isimujamii ili kuimarisha ujuzi wa kidijitali na hamu | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ya ujifunzaji,<br>• kueleza dhana ya sajili akiwa na wenzake,<br>• kutumia vyombo vya kidijitali katika kusakura na kueleza sifa za sajili mbalimbali (*k.v. sajili ya biashara, michezo, dini,* | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | *hotelini, n.k*),<br>• kuhakiki matini mbalimbali za Kiswahili na kubainisha sajili husika,<br>• kuigiza matumizi ya sajili mbalimbali darasani,<br>• kutathmini uigizaji wa wenzake kwa upendo na | |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | heshima,<br>• kutunga maswali dadisi yanayolenga sajili za lugha. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kupata maelezo kuhusu isimujamii.
- Hamu ya ujifunzaji na utafakuri – wakati mkurufunzi anapofanya utafiti ili kuwasilisha matokeo ya kazi mradi ya vikundi.
- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhikiana na wenzake ili kujadili majukumu ya lugha katika miktadha mbalimbali.
- Kujiamini – mkurufunzi anapoigiza matumizi yafaayo ya lugha katika miktadha mbalimbali.

**Maadili:**

- Umoja – mkurufunzi anaposhiriki katika kazi za vikundi.
- Uwajibikaji – mkurufunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia .
- Upendo – wakati wakurufunzi wanafanya kazi pamoja

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza dhana ya isimujamii. | Anaeleza dhana ya isimujamii kwa ufasaha na wepesi. | Anaeleza dhana ya isimujamii. | Anaeleza dhana ya isimujamii japo si kikamilifu. | Anaeleza dhana ya isimujamii kwa kusaidiwa. |
| Kutambua na kujadili majukumu mbalimbali ya lugha katika jamii. | Anatambua na kujadili majukumu mbalimbali ya lugha katika jamii ipasavyo na kwa urahisi. | Anatambua na kujadili majukumu mbalimbali ya lugha katika jamii ipasavyo. | Anatambua na kujadili baadhi ya majukumu ya lugha katika jamii ipasavyo. | Anatambua na kujadili baadhi ya majukumu ya lugha katika jamii kwa usaidizi wa wenzake. |
| Kuigiza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya kijamii. | Anaigiza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya  kijamii kwa usahihi na ubunifu mkubwa. | Anaigiza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya kijamii kwa usahihi. | Anaigiza matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ya  kijamii japo si kwa usahihi. | Anaigiza matumizi ya lugha katika miktadha ya  kijamii kwa usaidizi wa wenzake au mkufunzi. |
| Kufafanua sifa za sajili mbalimbali za lugha kupitia maigizo. | Anafafanua sifa za sajili kwa urahisi na ufasaha. | Anafafanua sifa za sajili mbalimbali za lugha. | Anafafanua sifa za baadhi ya sajili za lugha. | Anafafanua sifa chache sana za baadhi ya sajili za lugha. |
| Kuhakiki matini za Kiswahili na kubainisha sajili husika. | Ankuhakiki matini za Kiswahili na kubainisha sajili husika ipasavyo na kwa urahisi. | Ankuhakiki matini za Kiswahili na kubainisha sajili husika ipasavyo. | Ankuhakiki matini za Kiswahili na kubainisha baadhi ya  sajili husika. | Ankuhakiki  matini za Kiswahili na kubainisha baadhi ya sajili husika kwa kusaidiwa. |
| Kutumia sajili mbalimbali za lugha katika miktadha | Anatumia sajili mbalimbali za lugha katika miktadha tofauti | Anatumia sajili mbalimbali za lugha katika | Anatumia baadhi ya sajili za lugha katika miktadha tofauti ya | Anatumia baadhi ya sajili za lugha katika miktadha tofauti ya |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| tofauti ya kijamii ili kukuza umilisi wa kujiamini. | kwa ufasaha na kwa wepesi. | miktadha tofauti ya kijamii kwa ufasaha. | kijamii kwa ufasaha. | kijamii kwa usaidizi wa wenzake au mkufunzi. |
| Kutunga maswali dadisi yanayolenga sajili za lugha katika jamii. | Anatunga maswali dadisi yanayolenga sajili za lugha katika jamii kwa usahihi na ubunifu. | Anatunga maswali dadisi yanayolenga sajili za lugha katika jamii kwa usahihi. | Anatunga baadhi ya maswali dadisi yanayolenga sajili za lugha katika jamii kwa usahihi. | Anatunga maswali bila kuzingatia kanuni za udadisi. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1. Uchambuzi wa Mashairi (Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kueleza na kujadili aina na bahari mbalimbali za mashairi katika jamii,<br>b) kusoma na kuchambua mashairi ili kueleza maudhui na muundo,<br>c) kuandaa andao la somo la kufundishia mashairi katika gredi za juu za shule ya msingi,<br>d) Kutumia mbinu mbalimbali kufundishia ushairi,<br>e) kuthamini nafasi ya mashairi katika jamii. | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadiliana na wenzake aina na bahari mbalimbali za mashairi,<br>• kusoma aina mbalimbali za mashairi akiwa peke yake,<br>• kuchambua na kueleza maudhui na muundo wa shairi akiwa na wenzake,<br>• kuandaa andao la somo akizingatia mpangilio ufaao,<br>• kujadili na wenzake mbinu mbalimbali za kufundishia ushairi,<br>• kufanya mazoezi ya kufundishia mashairi kwa kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na kwa kuzingatia andao la somo alililoliandaa,<br>• kutathmini mazoezi ya wenzake kwa heshima na upendo. | Uchambuzi wa mashairi una umuhimu gani kwa wanafunzi wa shule ya msingi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Tathmini – mkurufunzi anapotathmini hoja za wenzake katika kikundi kuhusu uchambuzi wa maudhui na fani katika ushairi.
- Mawasiliano na ushirikiano mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi.
- Uraia na uongozi – mkurufunzi anapochukua majukumu mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapofanya mazoezi ya kutumia mbinu mbalimbali kufundishia ushairi.

DRAFT

| |
|---|
| • Kujiamini – mkurufunzi anapotumia mbinu mbalimbali kufundishia ushairi mbele ya wenzake. |
| **Maadili:**<br>• Uadilifu – mkurufunzi anapochambua mashairi yenye maudhui yanayokuza maadili.<br>• Upendo – wakurufunzi wanapotangamana katika kazi za vikundi.<br>• Umoja – mkurufunzi aoaposhirikiana na wenzake katika kazi za kikundi. |

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarijio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza na kujadili aina na bahari mbalimbali za mashairi katika jamii. | Anaeleza na kujadili aina na bahari mbalimbali za mashairi kwa usahihi na kwa urahisi. | Anaeleza na kujadili aina na bahari mbalimbali za mashairi | Anaeleza na kujadili baadhi ya aina na bahari za mashairi | Anaeleza bila kujadili aina na bahari mbalimbali za mashairi |
| Kusoma na kuchambua shairi ili kueleza maudhui na muundo. | Anasoma na kuchambua shairi ipasavyo na kwa kina. | Anasoma na kuchambua shairi ipasavyo. | Anasoma na kuchambua baadhi ya vipengele vya shairi. | Anasoma na kuchambua shairi kwa kusaidiwa na wenzake. |
| Kuandaa andao la somo la kufundishia mashairi kwa kuzingatia vipengele vifaavyo. | Anaandaa andao la somo la kufundishia mashairi akizingatia vipengele vifaavyo na kwa wepesi. | Anaandaa andao la somo la kufundishia mashairi akizingatia vipengele vifaavyo. | Anaandaa andao la somo la kufundishia mashairi akizingatia baadhi ya vipengele vifaavyo. | Anaandaa andao la somo la kufundishia mashairi bila kuzingatia mpangilio ufaao wa vipengele. |
| Kutumia mbinu mbalimbali kufundishia ushairi. | Anatumia mbinu mbalimbali kufundishia ushairi kikamilifu na kwa ufasaha. | Anatumia mbinu mbalimbali kufundishia ushairi kikamilifu. | Anatumia baadhi ya mbinu kufundishia ushairi. | Anatumia baadhi ya mbinu za kufundishia ushairi kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1. Uandishi wa Kazi za Kisanii (Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kazi za kisanii ili kuzitofautisha na kazi zingine za uandishi,<br>b) kufafanua madhumuni ya uandishi wa kazi za kisanii katika shule ya msingi,<br>c) kulinganisha na kutofautisha tanzu za fasihi andishi,<br>d) kujadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uandishi wa kazi ya kisanii,<br>e) kudhihirisha ubunifu wake kwa kutunga kazi ya kisanii,<br>f) kusoma na kuhariri kazi mbalimbali za kisanii,<br>g) kuonea fahari uandishi wa kazi ya kisanii | Mkurufunzi aweze:<br>• kueleza maana ya kazi za kisanii,<br>• kujadili madhumuni ya uandishi wa kazi za kisanii,<br>• kujadili tanzu za kazi za kisanii (*riwaya, tamthilia na ushairi*) na sifa zake,<br>• kulinganisha na kutofautisha tanzu za fasihi andishi kupitia utafiti wa maktabani na mtandaoni,<br>• kujadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uandishi wa kazi ya kisanii (*k.v. maudhui na fani*),<br>• kusakura mtandaoni ili kupata na kusoma kazi mbalimbali za kisanii,<br>• kufanya mradi wa kutunga kazi ya kisanii (*k.v. hadithi fupi, diwani ya mashairi, tamthilia, hadithi za watoto na kazi zingine zinazosheheni masuala mtambuko anuwai*), | 1. Kuna umuhimu gani kujifunza uandishi wa kazi za kisanii?<br>2. Ni mambo gani ya kuzingatia katika uandishi wa kazi ya kisanii? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | maishani. | • kuhariri kazi ya kisanii aliyoandika akishirikiana na wenzake,<br>• kujadiliana na wenzake kuhusu jinsi ya kuboresha uandishi wa kazi ya kisanii. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anaposakura mtandaoni ili kupata na kusoma kazi mbalimbali za kisanii.
- Tathmini – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kazi aliyotunga.
- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anapohariri kazi ya kisanii aliyoandika akishirikiana na wenzake.
- Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anapotunga kazi za kisanii.

**Maadili:**

- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za vikundi.
- Umoja – wakurufunzi wanaposhiriki katika kazi za vikundi kueleza maana na kujadiliana kuhusu mtiririko na mshikamano katika uandishi.
- Uwajibikaji – mkurufunzi anapoandika mtungo na kujadiliana na wenzake ili kutolewa maoni.
- Maadili mbalimbali yaliyolengwa katika kazi ya kisanii *k.v. uaminifu, upendo, uzalendo, uadilifu, amani na haki za kibinadamu*.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza maana ya kazi za kisanii kwa ufasaha. | Anaeleza maana ya kazi ya kisanii kwa ufasaha na urahisi. | Anaeleza maana ya kazi ya kisanii kwa ufasaha. | Anaeleza maana ya kazi ya kisanii japo si kwa ufasaha. | Anaeleza maana ya kazi ya kisanii kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kufafanua madhumuni ya uandishi wa kazi za kisanii kwa usahihi. | Anafafanua madhumuni ya uandishi wa kazi za kisanii kwa usahihi na wepesi. | Anafafanua madhumuni ya uandishi wa kazi za kisanii kwa usahihi. | Anafafanua baadhi ya madhumuni ya uandishi wa kazi za kisanii kwa usahihi. | Anafafanua baadhi ya madhumuni ya uandishi wa kazi za kisanii kwa kusaidiwa. |
| Kulinganisha na kutofautisha tanzu za fasihi andishi. | Analinganisha na kutofautisha tanzu za fasihi andishi ipasavyo na kwa ufasaha. | Analinganisha na kutofautisha tanzu za fasihi andishi ipasavyo. | Anatoa hoja chache kulinganisha na kutofautisha tanzu za fasihi andishi. | Analinganisha na kutofautisha baadhi ya tanzu za fasihi andishi kwa usaidizi wa wenzake. |
| Kujadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uandishi wa kazi ya kisanii. | Anajadili kwa ufasaha na wepesi mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uandishi wa kazi ya kisanii. | Anajadili kwa ufasaha mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uandishi wa kazi ya kisanii. | Anajadili kwa ufasaha baadhi ya mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uandishi wa kazi ya kisanii. | Anajadili bila ufasaha baadhi ya mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uandishi wa kazi ya kisanii. |
| Kutunga kazi ya kisanii kwa ubunifu. | Anatunga kazi ya kisanii kwa ubunifu na wepesi. | Anatunga kazi ya kisanii kwa ubunifu. | Anatunga kazi ya kisanii bila ubunifu mwingi. | Anatunga kazi yoyote ya kisanii kwa kusaidiwa. |
| Kusoma na kuhariri kazi za kisanii ifaavyo. | Anasoma na kuhariri kazi za kisanii kikamilifu na kwa wepesi. | Anasoma na kuhariri kazi za kisanii kikamilifu. | Anasoma na kuhariri baadhi ya kazi za kisanii kikamilifu. | Anasoma na kuhariri baadhi ya kazi za kisanii kwa kusaidiwa. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Muundo wa Sentensi ya Kiswahili**<br><br>**(Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo mkurufunzi aweze:<br>a) kubainisha muundo wa sentensi ya Kiswahili na kuufafanua<br>b) kuchanganua sentensi ya Kiswahili kwa mtindo wa matawi, visanduku na mishale ili kubainisha vipashio vyake<br>c) kuchangamkia uchanganuzi wa sentensi ya Kiswahili kama njia ya kuimarisha maarifa ya kitaaluma. | Mkurufunzi aweze:<br>• kubainisha vipashio vinavyounda sentensi kama vile Kundi Nomino na Kundi Tenzi,<br>• kufafanua miundo ya Kundi Nomino na Kundi Tenzi,<br>• kueleza mitindo ya uchanganuzi wa sentensi (*vielelezo matawi, visanduku na mishale*),<br>• kuchanganua sentensi za Kiswahili akiwa na wenzake (*k.v sahili, ambatano na changamano*) kwa kutumia mitindo iliyotajwa,<br>• kutumia vifaa vya kidijitali kuchanganua sentensi,<br>• kuwasilisha sentensi zilizochanganuliwa kwenye ubao na chati ili wengine wazitathmini,<br>• kutathmini sentensi zilizowasilishwa na wenzake. | Uchanganuzi wa sentensi una nafasi gani katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili? |

DRAFT

| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:** |
|---|
| • Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuchanganua sentensi.<br>• Tathmini – mkurufunzi anapowasilisha sentensi zilizochanganuliwa kwenye ubao na chati ili wengine wazitathmini. Pia, mkurufunzi anapotathmini sentensi zilizotungwa na wenzake.<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake kuchanganua sentensi. |
| **Maadili:** |
| • Uwajibikaji – mkurufunzi anaposhiriki katika kazi ya vikundi na kuwasilisha mbele ya wenzake.<br>• Umoja, upendo na heshima– mkurufunzi anaposhiriki pamoja na wenzake katika shughuli za vikundi huku akithamini na kuheshimu mchango wa wengine. |

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kubainisha muundo wa sentensi ya Kiswahili na kuufafanua. | Anabainisha muundo wa sentensi ya Kiswahili na kuufafanua kwa ufasaha na mtiririko wa kuvutia. | Anabainisha muundo wa sentensi ya Kiswahili na kuufafanua kwa ufasaha. | Anabainisha muundo wa sentensi ya Kiswahili bila kuufafanua. | Anabainisha muundo wa sentensi ya Kiswahili na kuufafanua kwa kiasi kwa kuelekezwa. |
| Kuchanganua sentensi ya Kiswahili kwa mtindo wa matawi, visanduku na mishale. | Anachanganua sentensi ya Kiswahili kwa mtindo wa matawi, visanduku na mishale kwa ufasaha na urahisi. | Anachanganua sentensi ya Kiswahili kwa mtindo wa matawi , visanduku na mishale kwa ufasaha. | Ana makosa machache katika kuchanganua sentensi ya Kiswahili kwa mtindo wa matawi, visanduku na mishale. | Ana makosa mengi katika kuchanganua sentensi ya Kiswahili kwa mtindo wa matawi , visanduku na mishale ili kubainisha vipashio vyake. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4. 2 Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa (Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo mkurufunzi aweze:<br>a) kueleza na kujadili usemi halisi na usemi wa taarifa katika mawasiliano,<br>b) kubadilisha usemi halisi hadi wa taarifa na wa taarifa hadi halisi ili kufanikisha mawasiliano,<br>c) kutumia mbinu mwafaka kufundishia usemi halisi na wa taarifa,<br>d) kuthamini matumizi fasaha ya usemi halisi na wa taarifa katika | Mkurufunzi aweze:<br>• kueleza maana ya usemi halisi na usemi wa taarifa,<br>• kujadili sifa za usemi halisi na usemi wa taarifa,<br>• kutafiti kuhusu sifa na matumizi ya usemi halisi na usemi wa taarifa maktabani na mtandaoni,<br>• kutunga na kuandika daftarini au kwenye kifaa cha kidijitali sentensi katika usemi halisi na wa taarifa,<br>• kutathmini sentensi halisi na za taarifa zilizotungwa na wenzake,<br>• kubadilisha usemi halisi kuwa wa taarifa na wa taarifa kuwa halisi,<br>• kutambua na kujadili na wenzake mbinu za kufundishia usemi halisi na wa taaarifa,<br>• kubainisha na kujadili mikakati ya kufundishia usemi halisi na wa taarifa,<br>• kuandaa nyenzo za kufundishia usemi halisi na wa taarifa,<br>• kutumia mbinu na mikakati ifaayo kufundishia usemi halisi na wa taarifa, | Ni mbinu zipi zinazoweza kutumika kufundishia usemi halisi na wa taarifa? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mawasiliano ya kila siku. | • kutathmini ufundishaji wake mwenyewe na wa wenzake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anaposhiriki katika mazoezi ya kufundisha usemi halisi na wa taarifa.
- Hamu ya ujifunzaji na utafakuri – mkurufunzi anapotafiti kuhusu sifa na matumizi ya usemi halisi na usemi wa taarifa maktabani na mtandaoni.
- Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anapofaragua, kuandaa na kutumia nyenzo zifaazo kufundishia usemi halisi na wa taarifa.
- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapofanya utafiti mtandaoni kuhusu sifa na matumizi ya usemi halisi na wa taarifa ili kujiimarisha kitaaluma.
- Kujiamini – mkurufunzi anapowasilisha funzo mbele ya wenzake darasani.

**Maadili:**

- Uwajibikaji – mkurufunzi anaposhiriki kikamilifu katika kazi za vikundi. Vile vile anapofanya utafiti maktabani na mtandaoni.
- Umoja, upendo na heshima – mkurufunzi anaposhiriki pamoja na wenzake katika shughuli za vikundi huku akithamini na kuheshimu mchango wa wengine.
- Uwajibikaji – mkurufunzi anapojiandaa ili kuwasilisha funzo kuhusu usemi halisi na wa taarifa.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kueleza na kujadili usemi halisi na usemi wa taarifa. | Anaeleza na kujadili usemi halisi na usemi wa taarifa kwa ufasaha na wepesi. | Anaeleza na kujadili usemi halisi na usemi wa taarifa kwa ufasaha. | Anaeleza na kujadili usemi halisi na usemi wa taarifa lakini maelezo yake si kamilifu. | Anaeleza bila kujadili usemi halisi na usemi wa taarifa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kubadilisha usemi halisi kuwa wa taarifa na wa taarifa kuwa halisi. | Anabadilisha usemi halisi kuwa wa taarifa na wa taarifa kuwa halisi kwa usahihi na wepesi. | Anabadilisha usemi halisi kuwa wa taarifa na wa taarifa kuwa halisi kwa usahihi. | Anabadilisha baadhi ya vifungu vya usemi halisi kuwa wa taarifa na wa taarifa kuwa halisi. | Anabadilisha baadhi ya vifungu vya usemi halisi kuwa wa taarifa na wa taarifa kuwa halisi akisaidiwa na mwalimu au wenzake. |
| Kutumia mbinu mwafaka kufundishia usemi halisi na wa taarifa. | Anatumia mbinu mwafaka kufundishia usemi halisi na wa taarifa kwa ufasaha na wepesi. | Anatumia mbinu mwafaka kufundishia usemi halisi na wa taarifa kwa ufasaha. | Anatumia baadhi ya mbinu mwafaka kufundishia usemi halisi na wa taarifa. | Anatumia baadhi ya mbinu mwafaka kufundishia usemi halisi na wa taarifa kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Vipengele vya Kusikiliza na Kuzungumza (Saa 4)** | Mkurufunzi aweze:<br>a) kutambua na kujadili vipengele mbalimbali vinavyohusu mada ya kusikiliza na kuzungumza katika ujifunzaji wa Kiswahili,<br>b) kujadili mbinu na mikakati ya kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza,<br>c) kutumia mbinu na mikakati mbalimbali ya kufundishia kusikiliza na kuzungumza<br>d) kuibua na kutumia nyenzo mbalimbali kufundishia kusikiliza na kuzungumza | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza katika ujifunzaji wa Kiswahili huku akiheshimu maoni ya wenzake (*k.v. Sauti [ala za kutamkia sauti], herufi na silabi, maamkuzi na maagano, maneno ya heshima na adabu, ufahamu sikizwa, maagizo, methali, mazungumzo, hadithi/masimulizi, vitendawili na mafumbo, vitanzandimi, misemo na nahau, tashbihi, sitiari, ushairi na nyimbo, mkujadiliano, hotuba, n.k*)<br>• kueleza mbinu na mikakati ya kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza *(k.v. Maswali na majibu, maigizo, maelezo, kuonyesha, mkujadiliano, nyimbo, wageni waalikwa, masimulizi, n.k)*<br>• kusakura kwenye tovuti kupata mbinu mbalimbali za kufundishia | Ni mbinu gani unazoweza kutumia kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td>e) kuonyesha jinsi ya kukuza umilisi wa mawasiliano na ushirikiano katika matumizi ya mbinu mbalimbali za kufundishia kusikiliza na kuzungumza<br>f) kuchangamkia matumizi ya mbinu na mikakati mbalimbali ya kufunzia mada mbalimbali za kusikiliza na kuzungumza ili kufanikisha shughuli ya ujifunzaji.</td><td>kusikiliza na kuzungumza kisha kuzijadili na wenzake,<br>• kuandaa shughuli ya ujifunzaji zinazoelekea kukuza umilisi wa mawasiliano na ushirikiano miongoni mwa wanafunzi,<br>• kuandaa shughuli za ujifunzaji zinayoonyesha jinsi ya kufundisha msamiati na kuiwasilisha kwa wenzake,<br>• kufanya mazoezi ya kutumia mbinu za kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza kwa uwajibikaji,<br>• kuandaa na kutumia nyenzo mbalimbali kufundisha kusikiliza na kuzungumza,<br>• kushirikiana na wenzake kutathminiana na kupima ufaafu wa mazoezi kwa mujibu wa mbinu za kufundishia.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:<br>• Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anaposhiriki katika mazoezi ya matumizi ya mbinu mbalimbali za kufunzia darasani.<br>• Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza matamshi ya sauti, kusakura maelezo kuhusu mbinu. za kufundishia kusikiliza na kuzungumza na pia uundaji wa nyenzo zinazotumiwa katika mazoezi ya</td></tr>
</table>

DRAFT

| |
|---|
| kufundisha darasani.<br>• Tathmini – mkurufunzi anapotathmini wenzake wanapofanya mazoezi ya matumizi ya mbinu na mikakati ya kufundishia kusikiliza na kuzungumza.<br>• Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhiriki na kuchangia kikamilifu katika mijadala. |
| **Maadili:**<br>• Umoja – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.<br>• Uwajibikaji – mkurufunzi anaposhiriki katika mazoezi ya kufundishia, kuunda na kutunza nyenzo.<br>• Heshima – mkurufunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi wanayofanya. |

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kujadili vipengele mbalimbali vinavyohusu mada ya kusikiliza na kuzungumza. | Anatambua na kujadili kwa wepesi vipengele mbalimbali vinavyohusu mada ya kusikiliza na kuzungumza. | Anatambua na kujadili vipengele mbalimbali vinavyohusu mada ya kusikiliza na kuzungumza. | Anatambua na kujadili baadhi ya vipengele vinavyohusu mada ya kusikiliza na kuzungumza. | Anatambua na kujadili vipengele mbalimbali vinavyohusu mada ya kusikiliza na kuzungumza kwa kusaidiwa. |
| Kueleza mbinu na mikakati ya kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza. | Anaeleza kwa kutoa mifano mbinu na mikakati ya kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza. | Anaeleza mbinu na mikakati ya kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza. | Anaeleza baadhi ya mbinu na mikakati ya kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza. | Anataja bila kueleza baadhi ya mbinu na mikakati ya kufundishia vipengele mbalimbali vya kusikiliza na kuzungumza. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia mbinu na mikakati mbalimbali ya kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anatumia kwa ustadi mbinu na mikakati mbalimbali ya kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anatumia mbinu na mikakati mbalimbali ya kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anatumia baadhi ya mbinu na mikakati ya kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anataja bila kutumia mbinu na mikakati mbalimbali ya kufundishia kusikiliza na kuzungumza. |
| Kuibua na kutumia nyenzo mbalimbali kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anaibua na kutumia kwa wepesi nyenzo mbalimbali kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anaibua na kutumia nyenzo mbalimbali kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anaibua na kutumia baadhi ya nyenzo kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anaibua na kutumia nyenzo za kufundishia kusikiliza na kuzungumza kwa usaidizi wa wenzake. |
| Kuonyesha jinsi ya kukuza umilisi wa mawasiliano na ushirikiano kwa kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia kusikiliza na kuzungumza.<br>. | Anaonyesha kwa wepesi jinsi ya kukuza umilisi wa mawasiliano na ushirikiano kwa kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anaonyesha jinsi ya kukuza umilisi wa mawasiliano na ushirikiano kwa kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anaonyesha jinsi ya kukuza umilisi wa mawasiliano na ushirikiano kwa kutumia baadhi ya mbinu za kufundishia kusikiliza na kuzungumza. | Anaonyesha jinsi ya kukuza umilisi wa mawasiliano na ushirikiano kwa kutumia mbinu mbalimbali za kufundishia kusikiliza na kuzungumza kwa kuelekezwa. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekzwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Uchambuzi wa Tamthilia (Tamthilia Teule)**<br><br>**(Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kutambua na kujadili sifa na dhima ya tamthilia katika jamii,<br>b) kuchambua tamthilia kwa kuzingatia vigezo husika katika fasihi,<br>c) kuonyesha jinsi usomaji wa fasihi unavyochangia katika uwazaji kina na utatuzi wa matatizo katika jamii,<br>d) kuchangamkia usomaji wa tamthilia na | Mkurufunzi aweze:<br>• kutambua na kujadili dhima ya tamthilia katika jamii,<br>• kujadili sifa za tamthilia (*k.v. kuhusu jukwaa, mazungumzo, wasanii, maleba, n.k.*) akiwa na wenzake katika kikundi,<br>• kujadili dhima ya tamthilia akiwa na wenzake,<br>• kutumia vifaa vya kidijitali kutazama maigizo ya tamthilia na kuykuhakiki,<br>• kuigiza sehemu za tamthilia katika kikundi,<br>• kutathmini maigizo ya makundi mengine na kuyatolea maoni,<br>• kujadili vigezo vya kuzingatia katika uchambuzi wa tamthilia kwa kushirikiana na wenzake,<br>• kusoma na kuchambua tamthilia kwa kushirikiana na wenzake kwa kurejelea maudhui na fani na kuwasilisha uchambuzi wake darasani ili wenzake wautathmini,<br>• kutathmini uchambuzi wa wenzake kwa heshima na upendo, | Uchambuzi wa tamthilia una nafasi gani katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | dhima yake katika jamii. | • kuigiza sehemu za tamthilia,<br>• kuhusisha maudhui ya tamthilia na maisha ya kila siku,<br>• kuonyesha jinsi usomaji wa fasihi unavyochangia katika uwazaji kina na utatuzi wa matatizo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Hamu ya ujifunzaji na utafakuri – mkurufunzi anapojadili dhima na sifa za tamthilia na maigizo.
- Kujiamini – mkurufunzi anapoweza kuwasilisha hoja zake katika kikundi.
- Mawasiliano na ushirikiano – mkurufunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili dhana ya tamthilia na maigizo.
- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutazama au kurekodi maigizo.

**Maadili:**

- Maadili mbalimbali kutokana na maudhui ya tamthilia na maigizo kama vile upendo, uwajibikaji, heshima, umoja, amani, uzalendo, haki za kijamii, uadilifu, n.k.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kujadili sifa na dhima ya tamthilia. | Anatambua na kujadili sifa na dhima ya tamthilia kwa ufasaha na utendeti. | Anatambua na kujadili sifa na dhima ya tamthilia kwa ufasaha. | Anatambua na kujadili sifa na dhima ya tamthilia bila ufasaha. | Anatambua lakini ana changamoto kujadili sifa na dhima ya tamthilia. |
| Kusoma na kuchambua tamthilia kwa kuzingatia vigezo husika. | Anasoma na kuchambua tamthilia kwa kuzingatia vigezo vyote husika | Anasoma na kuchambua tamthilia kwa kuzingatia vigezo vyote katika | Anasoma na kuchambua tamthilia kwa kuzingatia vigezo vingi husika. | Anasoma na kuchambua tamthilia kwa kuzingatia vigezo husika vichache sana. |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | kikamilifu na kwa ufasaha. | fasihi kikamilifu. | | |
| Kuonyesha jinsi usomaji wa fasihi unavyochangia katika uwazaji kina na utatuzi wa matatizo. | Anaonyesha kwa usahihi na wepesi jinsi usomaji wa fasihi unavyochangia katika uwazaji kina na utatuzi wa matatizo. | Anaonyesha kwa usahihi jinsi usomaji wa fasihi unavyochangia katika uwazaji kina na utatuzi wa matatizo. | Anaonyesha kwa kiasi jinsi usomaji wa fasihi unavyochangia katika uwazaji kina na utatuzi wa matatizo. | Anaonyesha kwa kiasi jinsi usomaji wa fasihi unavyochangia katika uwazaji kina na utatuzi wa matatizo kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Usahihishaji na Uhariri wa Maandishi (Saa 4)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mkurufunzi aweze:<br>a) kujadili dhana ya usahihishaji na uhariri katika uandishi,<br>b) kusahihisha insha akizingatia vigezo vya kimsingi vya usahihishaji katika shule ya msingi,<br>c) kujadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uhariri wa makala ya Kiswahili,<br>d) kuhariri matini kidijitali kwa kuzingatia vigezo husika katika Kiswahili,<br>e) kuthamini usahihishaji na uhariri wa makala mbalimbali. | Mkurufunzi aweze:<br>• kujadili dhana ya usahihishaji na uhariri wa maandishi,<br>• kujadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika usahihishaji wa insha (*k.v mada, maudhui, sarufi, mtindo, msamiati, mtiririko, uakifishaji, ujumbe, mpangilio, hijai, n.k*) akishirikiana na wenzake,<br>• kufanya mazoezi ya kusahihisha insha kwa uwajibikaji,<br>• kufanya mazoezi ya kuhariri matini au mswada wa kazi ya kisanii, *(matini yenyewe izingatie masuala mtambuko anuwai)*<br>• kuhariri matini au mswada wa kazi ya kisanii kwa kutumia vifaa vya kidijitali kama vile tarakilishi akiwa na wenzake. | Ni mambo gani yanayotiliwa maanani katika shughuli za usahihishaji na uhariri? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapojadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika usahihishaji wa insha.
- Tathmini – mkurufunzi anapofanya mazoezi ya kusahihisha insha.

DRAFT

| |
|---|
| • Kujiamini – mkurufunzi anapotambua mambo muhimu ya kuzingatia katika usahihishaji.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo – mkurufunzi anapotathmini na kufanya maamuzi ya utuzaji wa insha anaposahihisha. |
| **Maadili:**<br>• Umoja – mkurufunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu usahihishaji na uhariri wa maandishi.<br>• Uwajibikaji – mkurufunzi anaposahihisha insha za wenzake. |

**Vigezo na Viwango vya Kuzingatia katika Kumtathmini**

| Kiwango / Kigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kujadili dhana ya usahihishaji na uhariri katika uandishi. | Anajadili dhana ya usahihishaji na uhariri katika uandishi kwa ufasaha na urahisi. | Anajadili dhana ya usahihishaji na uhariri katika uandishi kwa ufasaha. | Anajadili kwa kiasi dhana ya usahihishaji na uhariri katika uandishi. | Anajadili dhana ya usahihishaji na uhariri katika uandishi kwa kuelekezwa. |
| Kusahihisha insha akizingatia vigezo vya kimsingi vya usahihishaji. | Anasahihisha insha akizingatia vigezo vyote vya kimsingi vya usahihishaji kwa usahihi na wepesi. | Anasahihisha insha akizingatia vigezo vyote vya kimsingi vya usahihishaji. | Anasahihisha insha akizingatia vigezo vingi vya kimsingi vya usahihishaji. | Anasahihisha insha akizingatia vigezo vichache sana vya kimsingi vya usahihishaji. |
| Kujadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uhariri wa makala. | Anajadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uhariri wa makala kikamilifu kwa urahisi. | Anajadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uhariri wa makala kikamilifu. | Anajadili baadhi ya mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uhariri wa makala. | Anajadili mambo ya kimsingi ya kuzingatia katika uhariri wa makala kwa kusaidiwa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kusahihisha na kuhariri matini kidijitali kwa kuzingatia vigezo husika katika Kiswahili. | Anasahihisha na kuhariri matini kidijitali kwa kuzingatia vigezo husika kikamilifu na kwa wepesi. | Anasahihisha na kuhariri matini kidijitali kwa kuzingatia vigezo husika kikamilifu. | Anasahihisha na kuhariri matini kidijitali kwa kuzingatia baadhi ya vigezo husika. | Anasahihisha na kuhariri matini kidijitali kwa kuzingatia vigezo husika kwa kuelekezwa. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Uundaji wa Maneno**<br><br>**(Saa 2)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo mkurufunzi aweze:<br>a) kutambua na kutathmini mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili<br>b) kujadili matatizo ya uundaji wa maneno na utatuzi wake katika lugha ya Kiswahili<br>c) kutumia maneno yaliyoundwa kwa mbinu mbalimbali katika mawasiliano<br>d) kuunda maswali dadisi kuhusu uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili<br>e) kuthamini mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. | Mkurufunzi aweze:<br>• kutathmini mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili (*k.v. unyambuaji*, *ufupishaji*, *uradidi*, *akronimi*, *uambatanishaji*, *kubuni*, *uhulutishaji*, *utohozi*, *tafsiri*, *n.k.*)<br>• kufanya utafiti kuhusu mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno maktabani na mtandaoni<br>• kutoa mifano ya maneno yaliyoundwa kwa kutumia mbinu mbalimbali<br>• kujadili matatizo ya uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili na utatuzi wake<br>• kutunga sentensi akitumia maneno yaliyoundwa kwa njia mbalimbali<br>• kuunda maswali dadisi kuhusu uundaji wa maneno akiwa na | Uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili unakabiliwa na changamoto zipi? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake katika kikundi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapotumia ujuzi wa mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno Kujiamini – mkurufunzi anapojiongezea maarifa kwa kushiriki kikamilifu katika funzo.
- Tathmini – mkurufunzi anapotathmini kazi yake na ya wenzake kuhusu uundaji wa maneno kwa kutumia mbinu mbalimbali.
- Hamu ya ujifunzaji na utafakuri – mkurufunzi anapowazia maneno mbalimbali na jinsi yalivyoundwa.

**Maadili:**

- Uwajibikaji – mkurufunzi anapofanya kazi ya kuunda maneno peke yake na katika vikundi.
- Uadilifu, umoja na heshima – mkurufunzi anapotagusana na kushirikina na wenzake katika shughuli za vikundi.

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kutambua na kutathmini mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anatambua na kutathmini mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na utendeti. | Anatambua na kutathmini mbinu mbalimbali za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. | Anatambua baadhi ya mbinu za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anatambua mbinu chache za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili akisaidiwa na mwalimu au wenzake. |
| Kujadili matatizo ya uundaji wa maneno na utatuzi wake. | Anajadili matatizo ya uundaji wa maneno na utatuzi wake kwa ufasaha na wepesi. | Anajadili matatizo ya uundaji wa maneno na utatuzi wake kwa ufasaha | Anajadili baadhi matatizo ya uundaji wa maneno na utatuzi wake. | Anajadili matatizo ya uundaji wa maneno na utatuzi wake kwa kuelekezwa. |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutumia maneno yaliyoundwa kwa mbinu mbalimbali katika mawasiliano. | Anatumia maneno yaliyoundwa kwa mbinu mbalimbali katika mawasiliano kwa usahihi na urahisi. | Anatumia maneno yaliyoundwa kwa mbinu mbalimbali katika mawasiliano. | Anatumia baadhi ya maneno yaliyoundwa kwa mbinu mbalimbali katika mawasiliano. | Anatumia maneno yaliyoundwa kwa mbinu mbalimbali katika mawasiliano kwa usaidizi wa wenzake. |
| Kuunda maswali dadisi kuhusu uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anaunda maswali dadisi kuhusu uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili kwa usahihi na wepesi. | Anaunda maswali dadisi kuhusu uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili kwa usahihi. | Anaunda baadhi ya maswali dadisi kuhusu uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anaunda maswali dadisi finyu na yasiyohusiana na uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.2 Mnyambuliko wa Vitenzi (Saa 3)** | Kufikia mwisho wa mada ndogo mkurufunzi aweze:<br>a) kubainisha na kunyambua vitenzi vya Kiswahili kwa mujibu wa kauli mbalimbali<br>b) kuunda matokeo maalum yanayotarajiwa ya kufundishia "Mnyambuliko wa Vitenzi" katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea,<br>c) kuandaa azimio la kazi la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea<br>d) kutayarisha andao la somo la kufundishia | Mkurufunzi aweze:<br>• kubainisha na kuigiza baadhi ya vitenzi anavyofahamu<br>• kufafanua dhana ya mnyambuliko wa vitenzi<br>• kubainisha kauli mbalimbali za vitenzi; *kutenda*, *kutendea*, *kutendwa*, *kutendesha*, *kutendewa*, *kutendeka*, *kutendeana* n.k.<br>• kunyambua vitenzi vya Kiswahili kwa mujibu wa kauli mbalimbali<br>• kubadilisha sentensi za Kiswahili kutoka kauli moja hadi nyingine akiwa na wenzake<br>• kutafiti kuhusu vitenzi maktabani na mtandaoni na kuwasilisha matokeo yake darasani<br>• kuunda matokeo maalum yanayotarajiwa ili kufundisha "Mnyambuliko wa Vitenzi" katika mojawapo ya gredi za juu za shule ya msingi | Mnyambuliko wa vitenzi una uamilifu gani katika Kiswahili sanifu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea,<br>e) kuonea fahari ujuzi wa mnyambuliko wa vitenzi katika mawasiliano ya kila siku. | • kuandaa azimio la kazi linaloweza kutumiwa kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi aliyoichagua<br>• kuandaa andao la somo kutokana na azimio la kazi alilolitayarisha<br>• kufanya mazoezi ya kufundishia mnyambuliko wa vitenzi ili wenzake wamtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Maarifa ya kufundishia – mkurufunzi anapopanua maarifa yake kuhusu vitenzi vya Kiswahili ili kujiendeleza kitaaluma. Pia, anaposhiriki katika mazoezi ya kufundishia mnyambuliko wa vitenzi na kuthamini matumizi ya mbinu na taratibu zifaazo.
- Ubunifu na uvumbuzi – mkurufunzi anapoigiza baadhi ya vitenzi na kwa mbinu za kiubunifu na pia anapoandaa na kutumia nyenzo zifaazo kufundishia mnyambuliko wa vitenzi.
- Ujuzi wa kidijitali – mkurufunzi anapofanya utafiti maktabani na mtandaoni kuhusu mnyambuliko wa vitenzi.
- Tathmini – mkurufunzi anapotathmini kazi yake na ya wenzake.

**Maadili:**

- Uwajibikaji – mkurufunzi anapotafiti kuhusu mnyambuliko wa vitenzi maktabani na mtandaoni. Mkurufunzi anapojiandaa ili kuwasilisha funzo kuhusu mnyambuliko wa vitenzi. Pia anaposhiriki katika kazi za vikundi huku akitekeleza wajibu wake ipasavyo.
- Umoja – mkurufunzi anaposhiriki pamoja na wenzake katika shughuli za vikundi huku akithamini
- Heshima – mkurufunzi anapoheshimu mchango wa wengine katika shughuli za kikundi.

DRAFT

**Viwango na Vigezo vya Kuzingatia katika Kutathmini**

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| Kubainisha na kunyambua vitenzi vya Kiswahili kwa mujibu wa kauli mbalimbali. | Anabainisha na kunyambua vitenzi vya Kiswahili kwa mujibu wa kauli mbalimbali ipasavyo na kwa urahisi . | Anabainisha na kunyambua vitenzi vya Kiswahili kwa mujibu wa kauli mbalimbali ipasavyo. | Anabainisha na kunyambua baadhi ya vitenzi vya Kiswahili kwa mujibu wa kauli mbalimbali. | Anabainisha na kunyambua vitenzi vya Kiswahili kwa mujibu wa kauli mbalimbali kwa kusaidiwa. |
| Kuunda matokeo maalum yanayotarajiwa ya kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. | Anaunda matokeo maalum yanayotarajiwa ya kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule na chekechea kwa usahihi na wepesi. | Anaunda matokeo maalum yanayotarajiwa ya kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea kwa usahihi. | Ana makosa machache katika kuunda matokeo maalum yanayotarajiwa ya kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. | Ana makosa mengi sana katika kuunda matokeo maalum yanayotarajiwa ya kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. |
| Kuandaa azimio la kazi la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. | Anaandaa kwa wepesi azimio la kazi la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. | Anaandaa azimio la kazi la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. | Anaandaa azimio la kazi la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi kwa kuzingatia baadhi ya sehemu za azimio la kazi. | Anaandaa azimio la kazi la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi kwa kuzingatia baadhi ya sehemu za azimio la kazi na kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kutayarisha andao la somo kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. | Anatayarisha kwa wepesi andao la somo la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. | Anatayarisha andao la somo la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. | Anatayarisha andao la somo la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya andao la somo. | Anatayarisha andao finyu sana la somo la kufundishia mnyambuliko wa vitenzi katika gredi za juu za shule ya msingi na chekechea. |